# *Ibrahimu Na Uzao Wake Baada Yake*

. . .ketini. Nina furaha sana kuwa hapa Chicago tena, ili, katika ushirika huu mkuu pamoja na Wafanyabiashara Wakristo wa Full Gospel, na ushirika wa watu, na kuwa pamoja nami, akinisaidia, na mmoja wa washirika wangu wakuu, na ndugu, Tommy Hicks. Nasi tuko chini ya matarajio makuu juma hili, kwa Bwana kutufanyia mambo makuu. Nami nasikia ya kwamba wamekuwa wakikutana kabla ya mkutano huu, na inaonekana kana kwamba kumekuwa na mambo makuu yaliyotimizwa, nasi tunatarajia makubwa zaidi, tunaposonga mbele kuelekea kwenye wakati wa mwisho.

2 Na sasa, tunapaswa kuwa hapa hadi Jumapili ijayo alasiri, naamini hiyo ni kweli. Wakati Ndugu Carlson alipotoa tu taarifa kwamba huduma hizi, yale yanayowabidi kupitia kufanya hizi huduma, ni kweli jinsi gani! Naye Ndugu Joseph akisimama karibu nami, akasema, "Vema," akasema, "kama wewe si askari, hupigwi risasi." Kwa hiyo nilifikiri hilo liliwekwa vizuri sana, hiyo—hiyo ni kweli.

3 Na wakati vita vikiendelea, mbona, unakuwa mlengwa shabaha halisi, kwa hiyo kuna jambo moja tu la kufanya, vaa silaha zote za imani, simama mwaminifu kwa Mungu, na usonge mbele, hivyo tu. Jeshi la Mungu halirudi nyuma, linaendelea mbele. Wengi wao huanguka kando, na kuanzisha *hili*, *lile*, ama *linginelo*, bali jeshi la Mungu linasonga mbele, tunaendelea mbele zaidi na zaidi.

4 Sasa, juma hili . . .Nilimtuma Billy yapata saa tisa, ama saa nane na nusu, naye akasema, alikaa mpaka saa tisa akaona watu wawili waliotaka kadi ya maombi, akasema walikuwa ni hao tu. Kwa hiyo, wakatangaza tutawaombea wagonjwa, sasa, kama, labda, Ndugu Hicks ana huduma kubwa ya kuwaombea wagonjwa, na labda tayari amefanya hivyo.

5 Na kama, kote katika juma hili sasa, nitamtuma Billy hapa, yapata saa kumi na mbili kila alasiri, ama kitu kama hicho, kugawa kadi za maombi, kama mtu yeyote, tukipata watu wanaotaka kuombewa, mimi, pamoja na Ndugu Hicks, na hao ndugu wengine, tutakuwa tukiwaombea wagonjwa juma zima; nasi tunamtarajia Mungu kujibu maombi yetu.

6 Katika miaka hii yote, sasa yapata miaka kumi na mitano katika huduma kote ulimwenguni, sijawahi kumponya mtu yeyote maishani mwangu mwote, lakini hakika nimekuwa na majibu mazuri sana ya maombi, ambapo Mungu amewaponya

wagonjwa, vilema, vipofu, na wanaoteseka, mpaka kweli imekuwa, kwangu mimi, moja ya . . . maisha yaliyojaa msisimko kwangu. Kama ningeitwa alasiri ya leo, ningemshukuru Mungu kwa kunifanya nijue jambo moja: Yesu Kristo ni Mwokozi wangu, kujua ya kwamba yu hai sasa, na hajafa bali amefufuka, na yu hai milele.

7 Na sasa, alasiri ya leo kabla hatujalikaribia Neno, kwa kuwa ninataka kutoa tamshi hili, kama mtaniwia radhi kwa muda kidogo tu kwa kusimama. Ninataka kujaribu kufanya jumbe zangu juma hili, fupi kidogo kuliko kawaida. Nina jina la kuhubiria popote kutoka saa moja hadi saa kumi, ama kitu kama hicho, lakini nitajaribu kuifanya kama dakika thelathini na tano, arobaini juma hili, Bwana akipenda. Kwa hiyo, watu, wengi wa watu ninaowajua, nafikiri, wanatoka mbali sana upande wa kusini, nafikiri hiyo ni kweli, chini *huko*, upande wa kusini, na kwa—kwa hiyo mnaweza kurudi kwa wakati mzuri, mrudi kwa ajili ya ibada inayofuata.

8 Sasa, kabla hatujalikaribia Neno, hebu na tumkaribie Mwandishi, kwa maombi, huku tukiinamisha vichwa vyetu.

9 Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru kwa ajili ya majaliwa ya kukusanyika pamoja, kwenye alasiri hii yenye mvua, katika Jina la Bwana Yesu, mara nyingine tena upande huu wa kuja Kwake, tukiamini ya kwamba siku moja tutakusanyika kwa mara yetu ya mwisho, mpaka mkutano ule mkuu utakapoitishwa Mbinguni. Majina yetu na yaandikwe wazi na dhahiri, huku yameoshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo, ambapo tunaweza kujibu orodha ya majina itakapoitwa, kwenye Karamu ya Arusi. Hiyo ndiyo sababu tuko hapa leo, Baba, ni kuitayarisha mioyo yetu kwa ajili ya tukio hilo kuu.

10 Tunaomba ya kwamba utusamehe kupungukiwa kwetu, makosa yetu, mambo ambayo tumefanya na kusema, ambayo hayakuwa sahihi. Tukumbuke tu, Baba, ya kwamba sisi ni wanadamu na tunakabiliwa na makosa ya kila namna. Na kama hatukuwa na ahadi Yako ya neema Yako, sote tungepotea, bali ni kwa neema Yako kwamba tumesimama leo kama askari, tukiamini kwa imani, ya kwamba Mungu ametuokoa na maisha ya dhambi, na kutoka kwenye adhabu ya Milele, katika ulimwengu wa baadaye.

11 Tunaomba sasa ya kwamba utakumbuka jitihada zetu zote, unajua ni kwa nini zimewekwa, unajua ni kwa nini tuko hapa, unajua vile nilivyomjibu Ndugu Carlson usiku ule kwenye simu, "Naam, najisikia kuongozwa." Sasa, Baba, hayo mengine yako mikononi Mwako, fanya nasi upendavyo. Kwa kuwa tunajiwasilisha Kwako pamoja na Neno Lako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

12 Katika Kitabu cha Wakolo-..., uh, Wagalatia, hasa, kwa ajili ya somo alasiri ya leo, ninataka kuchukua somo kutoka kwenye mlango wa 3 wa Wagalatia, na kifungu cha 29.

> Maana *mkiwa* ndani ya *Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, tena warithi sawasawa na ahadi.*

13 Na sasa, ninaliendea somo hili, alasiri ya leo, mara ya tatu ambapo, katika miezi miwili iliyopita, ambapo nimehubiri juu ya somo hili. Sababu ya mimi kufanya hivi ni kwa sababu nikiwazia ya kwamba—ya kwamba kama hatukuwa na ibada ya uponyaji, ningeweza kutenga muda kidogo zaidi kwa hili, kwa sababu, nionavyo mimi, ni mmoja wa zile jumbe kuu, muhimu sana kwa ajili ya saa hii tunayoishi.

14 Kwanza, ningetaka tu kuuliza swali hili: Ni wangapi waliopo hapa ambao ni Wakristo, Wakristo waliozaliwa mara ya pili? Inua mkono wako, kote jengoni, kila mahali. Ninaamini ni asilimia mia moja, kila mahali, Wakristo waliozaliwa mara ya pili.

15 M—mlinzi angeninii, mwajua, mimi si mmojawapo wa hawa wahubiri wa kujionyesha, nami ningeninii, laiti mngezima hizo taa kubwa, kama...kama tunaweza kufanya hivyo, nitalithamini sana. Si—sipendi hizi, kile wanachoita taa zenye nuru kali, na aina mbalimbali za taa, napenda tu Nuru ya Roho Mtakatifu, karibu ndiye Mmoja tu ninayeweza kuwazia, na hawa wengine kwa namna fulani hunifadhaisha kidogo.

16 Na kwa hiyo sasa, alasiri ya leo, mimi, mna Biblia zenu, na, labda, penseli na karatasi, ningetaka myaandike haya, na kuyachunguza ibada ikiisha, na katika juma lijalo. Sasa, ninaamini tumepangiwa hapa mpaka yapata wakati gani...? Mpaka saa kumi na mbili. Hiyo itaniruhusu kumaliza theluthi moja yake. Na kwa hiyo, halafu baadaye kidogo, labda tunaweza kuliingilia vizuri zaidi kidogo.

Sasa, asante, bwana. Hilo ni zuri sana, sana. Sasa mnaonekana bora zaidi.

17 Na—nataka kuchukua somo hili, ama ninii, kutoa kwenye somo hili muktadha ninaotumainia kuwa hivi: *Ibrahimu Na Uzao Wake Baada Yake*.

18 Sasa ningetaka kufanya...Naamini hizi ni spika kila upande hapa. Nami ninawatakeni mhakikishe mnayakumbuka haya. Nami nitaninii...Nina kurasa mbili za Maandiko zilizoandikwa hapa, ambazo ningetaka kuwarejelezea Maandiko haya, kwa sababu kwa kweli ninaamini, kwa moyo wangu wote, kwamba tunaishi tu kwenye alasiri ya wakati, wa kuzimika kwa Nuru za jioni, na ku—kuja kwa Kristo kumekaribia. Nami ninaamini kabisa, na Kibiblia ninaweza kuthibitisha hilo kwa Maandiko, pasipo shaka lolote, ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho.

19 Sasa, kama ninaweza kuwaridhisha nayo au la, sijui, lakini kwangu mimi, hakika inaniridhisha. Na kwa kuwa sina elimu ya kutosha, kwa hiyo ninayaendea Maandiko kwa mtazamo wa mfano, na zaidi sana kama mwainishaji, kufananisha yale yamekuwako, yatakayokuwako, kwa sababu tunajua ya kwamba Maandiko kila moja lina maana ambatani. Kwamba, kama vile katika Mathayo 3, ilisema, "Kutoka Misri nimemwita mwanangu," sasa, kama utafuatilia marejeo hayo nyuma, utaona ya kwamba ilimaanisha Yakobo, Mwanawe, na pia Yesu, Mwanawe.

20 Kwa hiyo katika kufananisha, tunaona ambapo Agano la Kale linawakilisha lile Jipya, na vivuli hivi vyote mbalimbali na mifano, kama vile mwe—mwezi na jua ni mfano wa Kristo na Kanisa. Na wakati jua likitua, mwezi huangaza jua lisipokuwepo, kama vile tu vile Mwana alivyoondoka duniani kwenda Utukufuni kwa Baba, ndipo Mwezi, Kanisa, linatoa Nuru. Na jinsi mwezi unavyopata nuru yake ni kuakisi nuru duniani, kama nuru ndogo.

21 Na mambo haya yote, huenda yakaonekana zaidi kama ya kitoto kwa wanatheolojia mashuhuri, lakini siamini ninazungumzia wengi mno wa hao, na kama—kama ninawazungumzia, basi samahani kwa njia yangu ya kijinga ya kujaribu kuliwasilisha. Lakini ningeomba ya kwamba ungelichunguza vizuri sana kabla hujalipinga kijeuri.

22 Sasa kwa Ibrahimu na Uzao wake, nitachukua upande huu *hapa* kuwa ni Ibrahimu, nichukue upande *huu*, kama hii spika, Uzao wake baada yake. Sasa, *hii* spika hapa inamwakilisha Ibrahimu, na *hii* spika inawakilisha Uzao wake baada yake.

23 Sasa, Biblia ilisema, hapa katika—katika Wagalatia 3:29, "Na kama ninyi ni wa Kristo, basi nyinyi ni Uzao wa Ibrahimu, na—na warithi sawasawa na ahadi." Sasa, sote tutakubali ya kwamba ile ahadi alipewa Ibrahimu. Nasi mara nyingi tumeshangaa, nami nimeliendea fungu hili katika mtazamo mwingine mbali na yale ninayokusudia alasiri ya leo. Nimeliendea katika njia ya imani kwa ajili ya Kanisa, waaminio, na kadhalika, kujenga imani juu ya uponyaji, lakini kwa kuwa alasiri ya leo, hawakufanya hivyo, hata mmoja, kwa ajili ya kadi, basi nikawazia lingenipa wakati wa kuelezea jambo hili, wakati tulipokuwa na nafasi.

24 Sasa, Ibrahimu, ninataka kusanyiko liseme pamoja nami, darasa lo—lote, kwamba nitawataka, kusema pamoja nami, upande *huu* ni Ibrahimu, "Ibrahimu na Uzao wake baada yake." Sasa, ahadi ilitolewa kwa Ibrahimu, na (kiunganishi kinachofunga sentensi), Ibrahimu *na* Uzao wake baada yake. Ndipo Maandiko yakasema, "Mkiwa katika Kristo, basi ninyi ni Uzao wa Ibrahimu." Hiyo ni kweli?

25 Sasa, tunaingiaje katika Kristo? Somo linaanzia kwenye hili: Tunakuwaje, Kristo? Ni wakati tunapokuwa, tunapokuwa Wakristo. Tunakuwaje Wakristo? Tunapojazwa na Roho wa Kristo, basi maisha yetu yanatawaliwa na Uzima wa Kristo, ulio ndani yetu.

26 Sasa, kama vile mzabibu ukizaa, ta—tawi la mzabibu, li—linazaa zabibu, nalo tawi la tikitimaji huzaa tikiti maji, basi kama Kristo yuko ndani yako, basi maisha ambayo Kristo aliishi, na kazi ambazo Kristo alifanya, utazifanya pia. Alisema hivyo katika Yohana Mtakatifu 14:7, ama :8, ninaamini ndipo, ilisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya, na nyingi kuliko hizi atazifanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba."

27 Sasa, ahadi iliyotolewa kwa Kristo, ama, kwa Ibrahimu, na Uzao wake, nasi tukiwa ndani ya Kristo ni Uzao wa Ibrahimu. Sasa, tunaingiaje ndani ya Kristo? Je, tunaingia ndani ya Kristo kwa kukiri? La. Je, tunaingia ndani yake, kwa Kristo kwa kujiunga na kanisa? La. Je, tunaingia ndani ya Kristo kwa ubatizo wa maji? La. Tunaingiaje ndani ya Kristo? Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 12, ilisema ya kwamba "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja," ambao ni Mwili wa Kristo. Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, na kuwa washiriki wa Mwili huu.

28 Sasa, tunakumbuka kwamba kwa huyu Roho Mtakatifu tunaingizwa katika Mwili wa Kristo na kuwekwa huru na hukumu za Mungu. Hatuwezi kuingia hukumuni baada ya wewe kuwa ndani ya Kristo, kwa sababu Kristo alichukua hukumu kwa ajili yako. Alisimama mahali hapo, kama tu Adamu. Hapo mwanzo Adamu hakudanganywa, na Timotheo wa Pili inatwambia hivyo, kasema, "Adamu hakudanganywa, bali Hawa, kwa kudanganywa akaingia katika hali ya kukosa."

29 Sasa, Adamu hakudanganywa, alijua yale hasa aliyokuwa akifanya, lakini Hawa alidanganywa, alidhani alikuwa akifanya yaliyo mema. Shetani alimpa yapata asilimia tisini na tano ya Injili safi, na asilimia hiyo nyingine tano ilitosha kuitupilia mbali hiyo. Kwa hiyo hatuna budi kuwa, si sehemu tu ya Injili, hatuna budi kuwa ni Injili tupu. Hatuna budi kuwa na Neno tupu, kwa kuwa mpinga-Kristo ni mhubiri wa Injili kwa sehemu, tunajua hilo, na kazi zake ni Injili kwa sehemu.

30 Yesu alisema, katika Mathayo 24:35, ya kwamba mpinga-Kristo, katika siku za mwisho, angefanana sana na Kristo halisi, hata ingewapoteza walio Wateule, kama yamkini. Nilimsikia Ndugu yetu Billy Graham akisema siku chache zilizopita, katika ujumbe, kwamba mpinga-Kristo alikuwa tayari amewadanganya walio Wateule, bali sivyo ilivyo. Ndugu Billy, mimi, bila kubishana na mwinjilisti mashuhuri kama

huyo, bali hawawezi (*Kama* yamkini, bali haiwezekani.), kwa sababu Kanisa lilichaguliwa kwa ajili ya wokovu wa Milele, wala hakuna kitu kinachoweza kuwatenganisha, Hao ni wa Kristo, na ni—ni hivyo. Wako katika Mwili wa Kristo, wala hakuna kitu kinachoweza kuwatenganisha. Na hiyo ni sehemu ya somo alasiri ya leo.

31 Sasa, tutakaribia tuone kile Ibrahimu alichokuwa, na halafu kile Uzao wake ungekuwa baada yake. Na sasa, ningetaka kusema hili sasa kwa heshima: Kanisa la kwanza ambalo, Kanisa la Kikristo, lililoanzishwa, lilianzishwa huko Yerusalemu kwenye Siku ya Pentekoste. Kila mwanatheolojia itamlazimu kukubaliana na hilo, kila mwanatheolojia hulirejesha kanisa lao kwenye wakati huo; kanisa Katoliki. Na ni kweli, kanisa Katoliki lilianza kwenye Siku ya Pentekoste, kweli kabisa.

32 Lakini huko chini katika yapata miaka mia mbili baadaye, miaka mia tatu baadaye, waliliacha hilo, wakaingia katika madhehebu. Ndipo wakaunda kanisa kubwa, la ulimwenguni kote, ambalo *Katoliki* linamaanisha "la ulimwenguni kote," na kutoka hapo wakaanza kuwa na uhalifa wa kimitume, na kumleta mtu mwingine kuchukua mahali pa Petro, na mapapa, wakaanza kuwaita maaskofu, na kuendelea na kuendelea. Nao kwa kweli walianzia Pentekoste, hiyo ni kweli, maana Ukristo wote ulianzia Pentekoste.

33 Sasa, jambo ambalo lanishangaza, kama wote tunaoamini kwamba tulianzia huko nyuma, basi kwa nini hatufanyi kama walivyofanya huko nyuma? Kwa nini hatuna baraka za Mungu juu ya Kanisa kama walivyokuwa nazo wakati huo? hebu tuwe Wakatoliki, ama chochote tulicho. Basi kwa nini hatuna Roho yeye yule, akitembea na kufanya kazi zile zile walizofanya huko nyuma? Je, ni kwa sababu tunapata *kitu kingine*, na kutulia juu yake, na kufanya fundisho kutoka kwake, na kipindi fulani, na kuliundia dhehebu, na kuliacha liendelee namna hiyo, kisha tunasema, "Sisi *hapa*!" Mungu huondoka moja kwa moja na kutuacha.

34 Hivyo ndivyo tu alivyowafanyia Katoliki, Lutheri, Presbiteri, Baptisti, Methodisti, na Wapentekoste, na kuendelea na kuendelea, Yeye amefanya jambo lile lile. Naye ataendelea kufanya hivyo, unapochora mstari na kusema, kwamba "Vema, tutajikusanya pamoja, na kujitenga na hao wengine." Biblia ilisema wangefanya hivyo katika siku za mwisho, wakionekana hawana imani. Na hiyo ni kweli. Tunataka imani iliyokuwako wakati mmoja.

35 Sasa, tunaanzia hapo, na tunajua ya kwamba huo ulikuwa ndio mwanzo wa Kanisa, na kwamba, hasa, hapo mwanzo wote walikuwa ni Wayahudi. Baada ya Wayahudi kueneza injili, ndipo ikaingia katika Warumi, na kwa Wayunani, na kadhalika, na kuanza, lakini yale matengenezo yakaja katika

ninii, huko nyuma katika miaka ya elfu moja mia tano ya mwanzoni, na hapo likaanza, kanisa la Kikristo, likaanza kujiundia madhehebu, ama kujikusanya pamoja, nasi tunaishi katika wakati wa mwisho wa kanisa sasa, Laodikia, kulingana na Maandiko.

36 Sasa, *huyo* ni Ibrahimu, *huu* ni Uzao wake baada yake. Sasa, fungueni mkitaka, katika Mwanzo 12, nasi tuanzie ambapo Mungu alimwita Ibrahimu. Na sasa, jambo la kwanza ninalotaka mjue, ya kwamba wakati Mungu, katika Mwanzo 12, alipomwita Ibrahimu, ilikuwa ni kwa uteuzi. Haikuwa kwa sababu ati Ibrahimu alikuwa mwema, haikuwa kwa sababu Ibrahimu alistahili jambo hilo, ilikuwa ni kwa sababu Mungu alimchagua Ibrahimu, sio Ibrahimu kumchagua Mungu, ilikuwa ni Mungu akimchagua Ibrahimu. Na hivyo ndivyo anavyomwita Mzao wake, pia, si vile unavyotaka kuwa, "si yeye atakaye, wala yeye apigaye mbio, bali Mungu arehemuye." Je, hayo ni Maandiko? Bila shaka. Si vile unavyotaka kuwa, ni vile Mungu amekuchagulia wewe kuwa.

37 Ibrahimu na Uzao wake baada yake, si *wazao*, sasa, *Uzao* baada yake, sasa, ule Uzao ulioahidiwa. Sasa, tunaona ya kwamba wakati Mungu alipomwita Ibrahimu, ilikuwa ni kwa uteuzi. Nimewasikia watu mara nyingi wakisema, "Nilimtafuta Mungu, nilimtafuta Mungu." La, sikubaliani nawe. Kamwe hukumtafuta Mungu, Mungu alikutafuta kwanza. Kamwe humtafuti Mungu, Mungu ndiye anayekutafuta. Wewe ndiwe ambaye hutajisalimisha kwa Mungu.

38 Ni kama tu vile kama ungeweza kumwambia nguruwe, katika zizi la nguruwe, ya kwamba—ya kwamba hapaswi kula takataka. Kama angeweza kuzungumza, angekwambia, "Mbona, wewe shika lako." Unaona? Mpaka asili yake itakapobadilishwa, basi daima atabaki nguruwe.

39 Daima unabaki kile ulicho, mwenye dhambi, kwa sababu umezaliwa katika dhambi, ukaumbika katika uovu, ukaja ulimwenguni ukisema uongo. Nawe ni mwenye dhambi kwa kuzaliwa. Basi, angalia yale Adamu aliyofanya, mara tu alipofanyika mwenye dhambi, kamwe hakujaribu kumtafuta Mungu, ilikuwa ni Mungu akimtafuta Adamu. Yeye kweli aliiwakilisha jamii ya binadamu papo hapo, wakati alipojificha nyuma ya majani ya mtini, ambayo alijitengenezea, kama vile watu wengi wanavyofanya siku hizi, "Mimi ni mfuasi wa kanisa, nami nimevaa aproni yangu ya jani la mtini." Lakini ilikuwa ni Mungu akimtafuta, Adamu, wala si Adamu akimtafuta Mungu.

40 Ilipaswa kuwa ni Adamu akipaza sauti, "Baba, Baba, uko wapi Wewe?" Badala yake, ilikuwa ni Mungu akisema, "Adamu, Adamu, uko wapi?" Na hilo ni jambo lile lile siku hizi, kwa hiyo hakuna hata chembe moja ya wema kwetu, kwamba tungeweza

kusema tulikuwa na uhusiano wowote na wokovu wetu. Ilikuwa ni Mungu akituita kwa uteuzi.

41 Sasa, nataka mweke akilini, kuhusu tatu. Nyakati zote kuna matabaka matatu ya watu duniani. Walitoka katika jamii tatu za watu, walitoka kwa Hamu, Shemu, na Yafethi. Tunajua ya kwamba Petro kwenye Siku ya Pentekoste, wakati Yesu alipokuwa amempa funguo za kuwafungulia Wayahudi Injili, halafu kwa Wasamaria, na kisha kwa Mataifa, hiyo ilikuwa, iliumaliza. Kulingana na Maandiko, jamii zote za dunia zilitokana na hao wavulana watatu.

42 Na sasa, kuna matabaka matatu ya watu ambayo daima yako katika kila kusanyiko, yamefanyizwa kila mahali, popote unapowapata, hao ni waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini. Unayapata hayo matabaka matatu ya watu labda katika kila kanisa lililopo ulimwenguni, ni wanaojifanya waaminio, na wasioamini, na waaminio.

43 Sasa, Ibrahimu, aliyeitwa kwa neema, sasa, Mungu hakusema, basi angalia, Mungu alipomwita Ibrahimu, Yeye hakusema, "Ibrahimu, *kama* utafanya jambo fulani, nitafanya jambo fulani." Alisema, "Ibrahimu, tayari nimefanya hivyo. Si yale uliyofanya, yale niliyofanya Mimi!" Yale Mungu aliyofanya, Yeye alisema.

44 Sasa, alipofanya agano na Adamu, "Kama hutaugusa mti huo, utaishi milele," Adamu akalivunja. Musa na hao wengine, "Mkizishika hizi amri, nita—nitafanya *hivi na vile*, kama mkivunja hizi amri, nitafanya *hivi na vile*." Mungu anapofanya agano na mwanadamu, mwanadamu huvunja agano lake na Mungu. Lakini ili kwamba Wateule, Kanisa, Watu walioteuliwa, kundi la Watu walioitwa watoke, waliotengwa wangekuwa na hakika ya kuokolewa, Mungu aliwaita kwa neema Yake.

45 Si kwamba Mungu angesema, "Ninakuchagua *wewe* na kukuhukumu *wewe*." Hasha. Lakini kama Yeye hana kikomo . . . Ni wangapi wanaoamini Yeye hana kikomo? Vema, basi Yeye alijua tangu mwa-. . . Alijua tangu mwanzo mwisho ungekuwaje. Hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo, Yeye yuko kila mahali, anajua yote, ana nguvu zote, wala hana kikomo.

46 Sasa, kama Yeye hana kikomo, kwa kujua Kwake tangu zamani, Yeye alijua ni nani angekuja Kwake, na ni nani asingekuja Kwake, Alijua ni nani angeokolewa na ni nani asingeokolewa. Hilo bila shaka lingeweka wazi Warumi 8 na 9 kwenu, kama kuna swali lolote kuhusu Mungu, kama Yeye huwaita watoto Wake kwa uteuzi ama la. Kwa kuwa hapo, Paulo akinena juu ya Esau na Yakobo, kabla hajazaliwa mtoto yeyote kati yao, bila hata kujua mema wala mabaya, Mungu alisema, "Ninampenda Yakobo na—na Esau ninamchukia," kabla mtoto yeyote kati yao hajapata nji—nji—njia ya kufanya chaguo. Lakini

Mungu alijua tangu mwanzo kile Esau alikuwa, Yeye alijua kile Yakobo alikuwa.

47 Naye Mungu alijua hapo mwanzo kile ulichokuwa, na kile usicho. Kwa hiyo, basi hatuwezi kuwa chochote ila kile . . . Kama hatuwezi kuwa kama mtu mwingine, hebu na tuwe tu kile Mungu alichotuumba, hivyo tu ndivyo tunavyoweza kufanya. Chochote mbali na hicho, ingekuwa ni unafiki, tungekuwa mnafiki, kwa hiyo hatutaki kuwa hivyo, ingekuwa bora, kuwa kafiri kuliko kuwa mnafiki. Hebu na tuwe tu kile tulicho.

48 Basi mambo haya yote hayana budi ku—hayana budi kufanya kazi pamoja kuyafanya magurudumu makuu ya Mungu kuendelea, wala hakuna hata jambo moja linaloenda kombo, nitawahakikishia hilo. Kila kitu . . . Mnafikiri ibilisi angeweza kamwe kumshinda Mungu? Jamani! La hasha. Kwa hiyo hawezi. Mungu, kila kitu, akikifanya kitende kazi kwa manufaa ya wale wampendao, Yeye anafanya tu kila kitu kiingie vizuri kabisa. Kitu pekee kinachomtatiza ni kuturudisha mstarini, mahali tunapopaswa kuwa, hapo ndipo Mungu anapopata shida Yake.

49 Sasa, Yeye alimwita Yakobo, si, uh, alimwita Ibrahimu, samahani, kwa uteuzi na kwa neema, na kumpa Uzima wa Milele, na kumwambia Yeye angemjia katika uzee, haikumbidi kufanya jambo moja juu yake. Jambo pekee, ilikuwa ni kwa neema, na hivyo ndivyo hasa Kanisa linavyoitwa siku hizi, ni kwa neema unaokolewa kwa njia ya imani, nasi tunajua hiyo ni kweli.

50 Mungu aliliita Kanisa kwa neema Yake. Kama isingalikuwa, leo, kwa ajili ya neema ya Mungu, ungekuwa hapa nje kwenye mvua ukiangalia mchezo wa mpira mahali fulani, ungekuwa hapa nje kwenye barabara kuu ukizunguka-zunguka, ungekuwa kwenye baa mahali fulani, ungekuwa huko nje na mke wa mtu fulani, ama mume wa mwanamke fulani, ungekuwa ninii, huko nje ulimwenguni, bali ni kwa wito na neema ya Mungu, kwamba Yeye amebadilisha nia zenu, akawafanya viumbe vipya katika Kristo Yesu, nayo nafsi yetu inamtazamia Yeye, leo, kwa matarajio ya kuja Kwake.

51 Kwa hiyo katika Wakolosai tunaona, Wakolosai 3, ilisema, "Msiambiane uongo, na mambo haya yote mliyokuwa mkifanya, wekeni mambo hayo kando, bila uovu, bila ugomvi, na kadhalika na kupendana. Kwa maana maisha yetu, tumekufa, maisha yetu yamefichwa katika Mungu kwa njia ya Kristo na kutiwa muhuri pale na Roho Mtakatifu. Na ndipo wakati Kristo, ambaye *ni* Uzima wetu, atakapoonekana, tutaonekana pamoja Naye." Loo, ni m—mtu wa jinsi gani . . . Yale lingeweza kumfanyia mwanamume ama mwanamke aliye na tumaini hilo linaloishi ndani yao leo, kuona ya kwamba tuko katika siku za mwisho, na kujua ya kwamba Uzima wetu, Kristo, atakapotokea,

tutaonekana hai pamoja Naye! Amina. Tunayo Arabuni yake sasa, kwa Roho Mtakatifu.

52 Mungu alimwita Ibrahimu, basi angalieni, wakati Mungu alipomwita Ibrahimu, Alimwita ajitenge na kutokuamini kwingine kwote. Haidhuru walikuwa wa kidini jinsi gani, jinsi walivyokuwa na kicho, jinsi walivyokuwa wazuri, Yeye aliagiza utengano mkamilifu. Naye Mungu, anapomwita mwanadamu, Yeye humwitia utengano mkamilifu, kama yeye ni Mzao wa Ibrahimu, kujitenga na mambo ya ulimwengu, na maisha haya ya kisasa.

53 Loo, wahudumu, leo, wana wakati mgumu sana wa kuwapeleka watu wao kwenye mkutano wa maombi Jumatano usiku, wa—wanapenda vipindi vya televisheni, na—na wanapenda burudani. Jumapili, hawataki kuja kanisani Jumapili, wengi wao. Wananiambia, wahudumu, ya kwamba viti vya kanisa ni vitupu, vinakuwa vitupu, kwa sababu watu wanaanza kwenda . . . Ulimwengu unatoa utabaka mwingi sana, na *madoido* mengi sana, na—na mapambo juu ya vitu vya ulimwengu, nao watu wanavutiwa nayo.

54 Sasa, hiyo inaonyesha ya kwamba kwanza kabisa, hawakuwa na kitu kwa kuanzia. Kwa kuwa kama unampenda Mungu, mimi . . . huwezi, usingeweza kujitenga na kanisa, wasingeweza kukufunga kwa mnyororo ukae mbali nalo, hawawezi kumficha mwaminio kutoka kwa Mungu.

55 Yeye, moyoni mwake, loo, huenda amedanganyika kabisa. Sasa, kuna watu wengi ambao kwa kweli wanafikiri kwamba wako sahihi, lakini kama ungesimama tu na kuyaangalia maisha yako, ungeona wao ni . . . Roho wa Mungu hayuko mle ndani. Kama hayaambatani na Biblia hii, basi kuna kasoro na huo ujuzi ulio nao. Kwa hiyo huna budi kurudi na kujiweka sawa na Neno upate kuona kama Uzima wa Mungu uko ndani yako.

56 Kama unaupenda ulimwengu kuliko unavyoupenda mkutano wa maombi, kama afadhali uangalie kipindi cha televisheni kuliko kuomba, una kasoro. Kama afadhali ufanye safari ya Jumapili alasiri badala ya kwenda kanisani, una kasoro mahali fulani, "Kwa sababu ulipo moyo wako, ndipo zilizipo hazina zako pia," alisema Bwana Yesu. Moyo wako umejengewa humo, wewe ni sehemu yake, unakuwa sehemu ya Kristo, kwa sababu umejengwa katika muundo wa Kristo, kwa sababu wewe ni Bibi-arusi wa Kristo, kama unampenda.

57 Sasa, Mungu alimwita kwa uteuzi, akampa agano katika Mwanzo mlango wa 12, sasa, tunataka kukumbuka hilo, na kuagiza utengano mkamilifu kutoka kwa mambo yote ya ulimwengu. Sasa, Ibrahimu hakumtii Mungu. Sasa, nitaita hilo . . .

58 Sasa, kama kuna . . . Kama nikizungumza neno moja hapa, alasiri ya leo, ambalo ni kinyume na imani ya mtu yeyote, vema

sasa, kamwe usiamke na kutoka nje, maana hiyo inaonyesha ulivyolelewa. Unaona? Lakini ninii tu, ni. . .Hebu niseme hivi: Ninaamini kama mtu ni Mkatoliki, naye analitegemea kanisa Katoliki kwa ajili ya wokovu, amepotea. Ninaamini kama mtu ni mfuasi wa kanisa Katoliki na anamtegemea Yesu Kristo kwa ajili ya wokovu, ameokoka. Kama yeye ni Mbaptisti, ama Mpentekoste, na analitegemea kanisa kwa ajili ya wokovu, amepotea. Kama anamtegemea Yesu Kristo, ameokolewa, kwa sababu kwa imani mnaokolewa kwa njia ya neema. Mnaona, imani ya—yako binafsi katika Kristo ndiyo inayokuokoa.

59 Wala hakuna kanisa linaloweza kukuokoa, hakuna dhehebu linaloweza kukuokoa, hakuna kundi la watu linaloweza kukuokoa, ni Kristo, na Yeye pekee, ambapo umeokoka. Na kwa hiyo, huna budi kukumbuka hilo. Kwa hiyo, sasa, kama nikigusa dhehebu fulani alasiri ya leo, ama kitu fulani ambacho—ambacho wewe ni mfuasi wake, tafadhali tulieni tu kidogo hapa, mpaka nitakapotoa hoja hii kwa ajili ya watu hawa, tafadhalini.

60 Sasa, tunaona ya kwamba kuhesabiwa haki, Mungu alimwita Ibrahimu kwa kuhesabiwa haki, na kwa neema alimwita, kwa uteuzi, alichaguliwa, kwa neema aliitwa na kupewa agano pamoja Naye. Kabla Ibrahimu hajasema neno moja kama ilikuwa ni kweli ama si kweli, kama angekubali, ama asingekubali, Mungu alimwita. Hiyo ni kweli? Sasa, someni cha kwanza, mlango wa 12 wa Mwanzo, cha kwanza, yapata vifungu kumi vya kwanza, ama kumi na vitano, nanyi mtalipata. Vema.

61 Sasa, halafu tunaona ya kwamba katika mlango wa 15 wa Mwanzo, sasa hiyvo ndivyo Mungu alivyomfanyia Ibrahimu jambo lingine. Sasa, tuliitaje ninii. . .? Alimwitaje Ibrahimu? Kwa imani, akamwita kwa neema, akamwokoa kwa neema, akamhesabia haki kwa neema. Hiyo ni kweli? Yeye aliliitaje Kanisa, Uzao wa Ibrahimu? Kwa imani, kwa neema, kuhesabiwa haki kwa neema, kwa imani, kama tu alivyomfanyia Ibrahimu, vivyo hivyo na Uzao wa Ibrahimu baada yake. Wote wanaoamini hilo waseme, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika. Huko hapo kuhesabiwa haki.

62 Sasa, ni kanisa gani lingewakilisha kuhesabiwa haki? Katika yale matengenezo ya kwanza kulikuwako na Martin Luther, aliyetokea akihubiri kuhesabiwa haki kwa imani, sisi sote tunajua hilo. Huyo kasisi kijana Mjerumani, aliyeutupa ushirika madhabahuni, na kusema ya kwamba haukuwa ni Damu ya Yesu Kristo, ama, ule mkate wa kosha, kwamba alijua ulikuwa ni mkate tu, na—na divai, kwa hiyo a—akautupa madhabahuni na kusema uliwakilisha mwili wa Kristo. Na hiyo ndiyo tofauti inayowatenganisha Wakatoliki na Waprotestanti. Mmoja alisema, Katoliki inasema, "*Ni* mwili wa Kristo." Na huyo mwingine akasema, "*Unawakilisha* mwili wa Kristo."

63 Sasa, Luther alisema, "Mwenye haki ataishi kwa imani." Na huo hasa ndio wito wa kwanza wa Uzao wa Ibrahimu baada ya yale mamia ya miaka ya nyakati za giza, kufanyiza Kanisa litakaloenda katika Unyakuo. Sasa, vumilieni kwa dakika moja. Sasa, Yeye alimwitaje Ibrahimu? Mwanzo 12 sasa, kwa imani, kuhesabiwa haki kwa imani, Yeye alimwita Uzao wa Ibrahimu tena, ambapo ilikuwa kwa imani, kwa kuhesabiwa haki.

64 Sasa, Ibrahimu hakumtii Mungu kikamilifu. Mpaka alipomtii Mungu kikamilifu, Mungu kamwe hakumthibitishia lile agano. Sasa, katika mlango wa 15 tunaona ya kwamba Yeye alithibitisha lile agano kwa Ibrahimu. Alifanyaje hilo? Angalieni, Yeye alimwambia Ibrahimu katika mlango wa 15, mtaona jambo hili: Kwamba Yeye alimwambia achukue ndama wa miaka mitatu, mbuzi, na kondoo, wa miaka mitatu, akawapasue vipande viwili, na kumtolea.

65 Naye Ibrahimu akawachukua hawa wanyama watatu wa miaka mitatu, kama nilivyowaambia, utengano mara tatu, hiyo tatu kama utatu, na kadhalika, hao watatu, sasa, tunaona ya kwamba aliwapasua hawa na kuwatenganisha. Kisha akawaweka wawili: hua, na mwana njiwa mle ndani, kamwe hakuwapasua hao ndege, kwa sababu kutoka Agano la Kale hadi Agano Jipya, damu ya dhabihu ilibadilishwa. Lakini hua na njiwa waliwakilisha uponyaji, kwa kuwa tunajua huo ulikuwa ni utakaso wa ukoma na kadhalika, kwa ajili ya uponyaji. Na uponyaji daima umejengwa juu ya imani yako katika Mungu. Basi kama nikisema . . .

66 Unasema, "Uponyaji haukujumuishwa katika Agano Jipya, katika ule upatanisho mpya."

67 Vema, kama ule upatanisho wa kale ulikuwa na uponyaji ndani yake, huu si ni bora zaidi? Ungewezaje kusema basi haukujumuishwa? Lakini yote yamewekewa msingi ule ule.

68 Kama vile Ndugu Hegre, ama baadhi ya hawa ndugu si muda mrefu uliopita, ndugu wa Kilutheri, ambao waliniambia walimjua mchawi aliyewaponya watu, nikasema, "La, hamjawahi. Hamjawahi kuona mchawi akimponya mtu." Hata hivyo, nimekuwa Afrika na kuwaona, kwamba wanaenda mbele ya mchawi na kuponywa. Katika La Salle, Lorraine, Ufaransa, kuna mahali huko, huko chini kwenye—kwenye ninii, huko karibu na, nafikiri ni Mto Seine, ambapo kanisa la Notre Dame, kuna mwanamke aliyekufa aliyezikwa hapo, pale mahali pakubwa mno paliposuguliwa ambapo wanaenda, na kupasugua wapate kuondoa mapigo mjini, jiwe hili kubwa juu ya mwanamke huyu aliyekufa. Mbona, bila shaka. Na mambo yanatukia. Hakika, ni mtazamo. Watu wanafikiri wanamwendea Mungu kupitia sanamu hiyo, watu wanafikiri wanamwendea Mungu kupitia kwa mchawi.

69 Na mara nyingi, watu hudumani leo hii hapa Marekani, watu husema, “Njoo tu, loo, ni—nina uponyaji.” Hilo—hilo ni kosa. Walimu wazuri, imara wa Injili hawafundishi namna hiyo, wanalifundisha kama katika ule upatanisho Kristo alikuponya. Nao wako hapa, kama tu watu wa Mungu, ni imani, kuamini na kukuombea. Lakini unapomsikia mtu fulani akisema, “Ninaweza kukuponya, nina uponyaji, nimefanya *hivi*,” hilo ni kosa. Kristo alifanya hivyo kwa ajili yako wakati alipokufa pale Kalvari kwa ajili yako. Hiyo ni baraka ambayo ni yako. Ni ninii yako . . .

70 Nao watu hawa wanaziendea sanamu hizi, na mifano, na wachawi, na wapiga ramli, na mambo hayo yote mbalimbali namna hiyo, wanaponywa kwa sababu wameamini ya kwamba kupitia hapo, wanamwendea Mungu, na uponyaji wa Kiungu umewekewa msingi juu ya—juu ya imani, kama unaamini.

71 Sasa, hiyo ndiyo sababu hua na njiwa hawakupasuliwa. Niliwaambia siku moja ningeweza kulifikia hilo, nami nikawazia kuwa na wakati mwingi kadiri nilio nao alasiri ya leo, ningejaribu kulifikia kwa ajili yenu. Hiyo ndiyo sababu haikuwa hivyo, hawakupasuliwa. Lakini hao wengine walipasuliwa, wakakatwa vipande viwili.

72 Sasa, Mungu alikuwa akifanya nini? Kuwaua wanyama hawa, ilihitaji damu, kusudi kuwe na dhabihu ya utakaso wa dhambi, inabidi kuwe na sadaka ya damu. Mungu aliweka msingi huo katika Mwanzo, wakati mwanadamu alipojaribu kujijengea madhehebu, ama namna fulani ya nguo ya majani ya mtini, na kulikwepa, Mungu alikataa kumwangalia.

73 Naye Mungu, wakati Mungu anapotoa ta—tamshi, wakati Mungu anaposema jambo lolote, wakati Mungu anapoitwa jukwaani kufanya uamuzi, uamuzi huo anaofanya hauna budi kudumu Milele, kwa sababu Neno Lake ni kamilifu. Hawezi kurudi nyuma na kusema, “Nilikosea jana, ninajua zaidi kulihusu leo.” Anawezaje kuwa asiye na kikomo hu—huku akitoa tamshi, na—na halafu imbidi kulighairi? Vipi? Hilo linatupa matumaini katika Yule tunayenena habari zake, Mungu, Yeye hawezi kushindwa.

74 Kama Mungu aliwahi kuitwa kumponya mgonjwa, Naye akamponya juu ya msingi wa imani yake, kama mtu mwingine akija kwenye misingi ile ile, Yeye hana budi kutimiza masharti yayo hayo, la sivyo alikosea wakati alipomponya mtu wa kwanza. Bila shaka.

75 Kama alimwokoa mtu kwa msingi wa imani, basi tutaingiaje basi juu ya kujiunga na kanisa, na kunyunyiziwa, na mabatizo, na kadhalika? Ni kwa imani, kwa neema, kwa nguvu. Mungu, kwa kitu ambacho ulikuwa . . . kitu ambacho ulitimiza masharti ya Mungu, Naye alikuita na kubadilisha maisha yako kabla hata hujaweza kufanya lolote kulihusu.

76 Mbona, hamna kitu ndani yako, kwanza kabisa wewe ni mwenye dhambi, wala hakuna kitu hapo cha kubadilisha, kwa hiyo Mungu, kwa neema Yake, alikujua tangu zamani, akakuita kwenye huduma Yake, na kwenye Karamu Yake ya Arusi. Unaona, hakuna kitu unachoweza kufanya hata kidogo. Kwa jumla ni neema ya Mungu, Mungu alifanya hivyo kwa neema. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka," si anayejifanya anaamini, bali, "anayemwamini Yeye aliyenipeleka, ana," wakati uliopo, "Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Amina.

77 Tutakwepaje hilo? Kuna imani nyingi sana ya kujifanya, kushikwa na mihemuko na mambo mbalimbali namna hiyo, lakini wakati moyoni mwako unaliamini, wakati jambo fulani limekupata, ambalo Mungu alilifanya, na Mungu Ndiye pekee anayeweza kufanya hivyo, kwa hiyo Mungu, kwa neema na kuteuliwa, aliweka hilo moyoni mwako upate kuliamini. Kwanza kabisa halikuwapo, wala hukuwa na njia ya kuliweka pale, Mungu aliliweka pale, nawe ukaitikia huo wito.

78 Sasa, angalieni, katika Mwanzo mlango wa 15, wakati alipomfundisha Ibrahimu ule utengano, wakati Ibrahimu alipokuwa tayari kujitenga, kutoka kwa Lutu asiyeamini, yule mshiriki vuguvugu wa kanisa, wakati Lutu aliposhuka kwenda Sodoma, na—na akawa meya wa huo mji, na kujijengea kanisa zuri huko chini, ama chochote kile, chochote alichofanya, ndipo Mungu akakutana na Ibrahimu, nao wakatoa dhabihu ya damu kwa ajili ya utengano, na kuthibitisha agano kwa Ibrahimu. Amina. Kwa kuwa pasipo kumwagwa kwa damu hakuna kutengwa na dhambi, mnaona, ni kupitia damu iliyomwagika.

79 Sasa, angalieni kile Yeye. . .kile kilichotukia, Yeye aliwachukua wanyama na kuwakata vipande. Ibrahimu alishika doria mpaka jua likatua, na kulikuwa na u—usingizi mzito uliomshika Ibrahimu. Ndipo alipoona usingizi mzito ukija, huo ulimaanisha mauti, ni kwa ajili yetu sote, sote tunakuja huko kwenye usingizi huo mkuu, wa Milele.

80 Sasa, tuliona mara baada ya hayo, akatazama mbele yake, na hofu kuu ya weusi na tanuru ya moshi. Ni kitu gani? Kuzimu. Kupitia katika bonde la uvuli wa mauti, kila mtu anaingia kuzimuni, huko ndiko kwake, na kisha mbele tu ya huo ikatokea Nuru ndogo nyeupe, iliyoingia katikati ya kila kimoja cha vipande hivyo vya nyama vilivyopasuliwa. Ibrahimu akiwa amethibitishiwa agano na Bwana Mungu, jinsi ambavyo alikuwa anaenda kumchukua Ibrahimu na kumfanya baba wa mataifa, jinsi alivyokuwa anaenda kumwokoa Ibrahimu na Uzao wake, alikuwa akifanya thibitisho la agano kwa damu iliyomwagika ya wanyama safi, waliotolewa sadaka.

81 Sasa, tunafanyaje agano? Tuseme kwa mfano, Ndugu

Carlson hapa, simama, kwa dakika moja, Ndugu Carlson, kama ningesema, Ndugu Carlson aseme, "Ndugu Branham, utakuja Miami kuninii, mkutanoni?"

82 Ningesema, "Vema, hebu tuliwazie, Ndugu Carlson." Ningesema, "Vema, ninaamini nitakuja. Vema, nitakuja, Ndugu Carlson. Nipe mkono." Mnaona? Hilo ni agano. "Tutakuwa kule." Hiyo ni kweli. Hiyo imetosha. Mnaona? Tutafanya agano namna hiyo. Hivyo ndivyo tunavyofanya agano.

83 Jinsi gani. . .? Mnajua huko Japan jinsi wanavyofanya agano? Wanatoka nje. . .Tunatoka kwenda kula, kwa kawaida. Wajapani wanachukua chupa ndogo ya chumvi, na kurushiana chumvi kidogo, hivyo ndivyo wanavyofanya agano mmoja na mwingine, maana chumvi ni kiunganishi, ni ladha, mnaona. Kwa hiyo wanarushiana chumvi, wakifanya agano.

84 Lakini katika siku za Ibrahimu, mnajua jinsi walivyofanya agano huko nyuma katika nchi za mashariki ya kimashariki wakati huo? Walimchinja mnyama kisha wakasimama katikati ya vipande hivi vya mzoga wa mnyama, waliandika kwenye karatasi ya ngozi, ama ngozi ya huyo mwana-kondoo, yeyote yule, na kufanya maandishi haya ya Kiyahudi, lile agano, chochote kile. Halafu basi, wao, juu ya mzoga wa mnyama huyu aliyekufa wakala kiapo, kwamba kama wakilivunja agano hili, na wakatwe vipande-vipande, kama vile mnyama huyu aliyekufa alivyokatwa. Ndipo wakaichukua hiyo ngozi na kuipasua, basi mmoja akaweka kipande kimoja, mmoja akaweka hicho kipande kingine. Ndipo basi wakati agano hili liliporudishwa, ama, wakati lile agano lilipotimia, basi vipande hivi viwili ilibidi viumane, na kuifanya ngozi hiyo na hizo herufi kuambatana, herufi kwa herufi.

85 Hivyo ndivyo hilo agano lilivyothibitishwa kwa Ibrahimu. Ambapo, Yeye alikuwa akionyesha mle ndani kile atakachofanya, katika nyakati zijazo, kwa Uzao wa Kifalme ambao alikuwa amemwahidi, hata hivyo yeye akiwa hana watoto. Alikuwa amemwahidi mwana, kwamba atampata. Alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano, naye Sara alikuwa na sitini na mitano wakati hiyo ahadi ilipotolewa, na ilikuwa miaka ishirini na mitano baadaye kabla hi—hiyo ahadi haijatimizwa. Lakini Mungu alimtimizia ahadi Yake, kwa sababu Ibrahimu aliendelea kumwamini Mungu.

86 Sasa, wakati wote, badala ya kuwa dhaifu, Ibrahimu alipata nguvu zaidi, Biblia ilisema. Alikuwa na nguvu zaidi, akimsifu Mungu, alijua itatendeka. Haidhuru inakawia muda gani, itatukia, itatukia.

87 Kama vile watu siku hizi, wanasema, "Loo," Biblia ilisema walisema, "Hakuna tofauti na wakati baba zetu walipolala. Loo, nimesikia huko 'kuja kwa Bwana' tangu nilipokuwa mtoto mdogo, mama yangu alisema alimsikia mama yake

akizungumzia jambo hilo, hakuna kitu kama hicho." Mnaona, ndipo wanaondoka wanaenda kula, kunywa, na kufurahi. Mnaona hilo? Wanaondoka na kuanza kwenda, kwa sababu gani? Hakujawahi kuwa na thibitisho lolote la jambo hilo moyoni mwao bado.

88 Lakini wakati Mungu akiisha kuthibitisha hilo moyoni mwako, badala ya kupa-. . .iwapo wewe ni Mzao halisi, wa kweli wa Ibrahimu, badala ya kuwa mnyonge kadiri unavyoona siku zikienda, utaendelea kuwa na nguvu zaidi wakati wote. Unasema, "Vema, kama nyanya hakuiona, na mama hakuiona, nisipoiona, nitakuwa nikiitazamia. Na nisipoiona, watoto wangu wataiona. Tunaninii, ninaamini hilo. Nikilala usingizi katika zamu ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita, ama ya saba," ama wakati wowote ule wa kanisa, wakati wa kwanza wa kanisa, ama hata wakati wa mwisho wa kanisa, hizo zamu, ambazo ni zamu, "Kama nikilala katika kila moja ya hizo, haidhuru ni wapi, nitaamka katika Yeye asubuhi hiyo. Kwa hiyo nitakuwa tayari, nikiamini ya kwamba Yeye anakuja katika wakati huu."

89 Sasa, lakini wakati anapozembea, na kusema, "Vema, nime—vema, nimesikia upuuzi huo," na kuendelea, unaona, si Uzao wa Ibrahimu. Uzao wa Ibrahimu haughairi. Hawaendi huku na huko, na kuingia na kutoka, na kurudi nyuma siku moja, na kwenda kanisani kesho yake, kisha kurudi, wanakaa sawa. Ndugu, wako ndani ya Kristo, nao hao hapo wamesimama, hakuna kitu kinachoweza kuwatikisa. Mbona Yesu alisema, "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, malango ya kuzimu hayawezi kulishinda." Mungu tayari amefanya agano na Ibrahimu na Uzao wake baada yake, na Kanisa hilo litakuweko bila waa wala kunyanzi, unaweza tu kutegemea hilo.

90 Kwa hiyo, mnaona, hizi, kipande hiki cha nguo, ama—ama kitambaa, kilikuwa katika siku hizo, si nguo, bali ngozi, iliraruliwa vipande, mtu mmoja akachukua kipande kimoja, huyo mwingine akachukua hicho kipande kingine. Ndipo wakati agano hili lilipotimia, basi walikutana, wala hakuna njia ya kuliigiza, kwa sababu vipande hivi viwili vilipaswa kuwa sawa kabisa katika ngozi na pia katika ma—maandishi, ilibidi yaambatane herufi kwa herufi.

91 Sasa, hivyo ndivyo hasa Mungu alivyofanya kwa Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu. Sasa, ninajua Isaka alikuwa Mzao wa Ibrahimu, kwa uwezekano, vema, ulikuwa ni uzao wa kawaida wa Ibrahimu, bali sio Uzao halisi wa Ibrahimu, ule Uzao halisi wa Ibrahimu ulikuwa ni Kristo, Uzao wa Kifalme. Isaka alikuwa tu ni kibadala mpaka Kristo alipokuja, ambaye alikuwa ni Mzao wa Ibrahimu. Sasa, halafu Mzao halisi wa Ibrahimu anaamini ile ahadi, kama tu vile Ibrahimu alivyofanya, kwa sababu ni kwa Ibrahimu na Uzao wake baada yake.

92 Sasa, angalia kile Mungu alichoufanyia ule Uzao wa Kifalme kufanya lile agano lithibitishwe: Alimchukua Kristo, ambaye alikuwa Mzao wa Ibrahimu, pale Kalvari akampasua vipande viwili. Akaondoa Roho Kwake, na kuuweka mwili Wake kaburini, na Nafsi Yake katika kuzimu, na kumfufua katika siku ya tatu, na kuufufua mwili Wake, kisha akauleta Utukufuni, na hapo akamshusha Roho, na kuuweka mwili kwenye mkono Wake wa kuume, akamshusha Roho, apate kuishi Kanisani, kulifanya Kanisa liwe na Uhai wa Kristo sana mpaka kwenye ule ufufuo, hao Wawili wataungana pamoja, Bibi-arusi na Bwana-arusi, kanisa na Kristo watafanana kabisa kwa ajili ya huduma ya namna ile ile, nguvu za namna ile ile, Roho wa namna ile ile. Aliufufua mwili wa Yesu Kristo na kuuweka kwenye mkono Wake wa kuume, mkono Wake wa kuume, na kulimwagia Kanisa Roho Mtakatifu kwenye Siku ya Pentekoste. Hivyo ndivyo Mungu alivyothibitisha agano Lake na Kanisa Lake.

93 Ndipo Yesu akasema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Nasi tunaona ya kwamba hiyo ndiyo njia ya Mungu aliyothibitishia agano Lake pamoja na Kanisa Lake, amina, kwa toleo la Damu, kwa Damu ya Yesu Kristo.

94 Sasa, Yeye alilitakasa Kanisa hilo basi, akalitakasa, akalitenganisha. Na wakati utengano unapokuja... Linamaanisha "kuwekwa kando." Ninii...Kwa kweli Neno *takasa* ni neno la Kiyunani, ambatani, ambalo linamaanisha "kutakaswa, kusafishwa, na kutengwa kwa ajili ya matumizi." Sasa, madhabahu ilikitakasa hicho chombo, kisha wakakitenga kwa ajili ya matumizi.

95 Kwa hiyo kile—kile...? Ni mjumbe aliyefuata aliyehubiri kuhesabiwa haki duniani? Luther, kwa ule Uzao. Ujumbe uliofuata ulikuwa ni upi? Wesley, Wamethodisti walihubiri utakaso, kazi ya pili dhahiri ya neema. Tunaona...Sote tunajua hilo, tunajua hilo.

96 Sasa, angalieni, yale aliyomfanyia Ibrahimu kwa kuhesabiwa haki, aliufanyia Uzao wake. Yale aliyomfanyia Ibrahimu kwa utakaso, utengano alipofanya hivyo, Yeye alifanya jambo lile lile. Wakati Kanisa linapojitenga Lenyewe na mambo yote ya ulimwengu, basi Mungu hulipaka Damu.

97 Sasa, ndipo anapofanya hivyo, basi huninii, huvuti sigara tena, kunywa pombe, hakuna tena mambo haya ya kuzurura-zura, kufanya yasiyofaa, ninyi ni watu waliotengwa. Hiyo ni kweli. Mungu anawatenganisha ninyi kama watu wa kipekee, imani nyingi za kujifanya zinaendelea katika mambo haya yote, lakini hata hivyo, lile Kanisa halisi, la kweli, ninazungumza juu ya U—Uzao halisi wa Ibrahimu, ule ambao kweli ni Uzao.

98 Sasa, angalieni jambo lingine alilofanya. Ndipo, baada ya kufanya hivyo, tunaona, sasa, je, Yeye alimwita Ibrahimu kwa

neema? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Je, aliliita Kanisa Lake kwa neema? “Amina.” Je, alizitakasa kazi za Ibrahimu kwa ninii...kwa sadaka ya damu? “Amina.” Je, alifanya jambo lile lile hapa nyuma kupitia kwa Wesley? “Amina.”

99 Sasa, sasa, katika mlango wa 17 wa Mwanzo, fungueni mla-...kifungu cha kwanza, Mungu anamtokea Ibrahimu katika Jina la—la Mwenyezi Mungu, ambalo neno la Kiebrania linamaanisha “El-Shadai.” *El* maana yake ni, “titi,” na, ama, *El* maana yake, “Mwenye nguvu,” na *Shad* maana yake ni, “titi,” kama titi la mwanamke, nalo *Shadai* ni “mwenye matiti.” “Ibrahimu, una umri wa miaka tisini na tisa,” wazia hilo, “nawe umepitia katika kuhesabiwa haki, umepitia utakaso, na sasa ninaonekana kwako kama Mungu mwenye nguvu, mwenye matiti.” Amina.

100 Sasa, kwa maneno mengine, “Ibrahimu, wewe, uhai wa—wako umekufa, kuhusu hilo, uhai wa mwili wako umekufa.” Kufa kwa tumbo la uzazi la Sara, ha—halikuwa...alikuwa tasa kwanza kabisa, na sasa angalia jinsi alivyo mkongwe sasa, yeye, kama mwanamume ana tisini na tisa, mwanamke ana themanini na tisa. Na kwa hiyo, “Sasa, angalia jinsi ulivyo mkongwe, na angalia jinsi Sara alivyo mkongwe, bali Mimi ndimi Mwenye nguvu, nijitoaye Mwenyewe kwako, lala kifuani Mwangu ukanyonye, Uhai Wangu Mwenyewe ndani yako. Mimi, kwa kuingiza Uhai Wangu ndani yako, nitakupa nguvu kwa ajili ya mwana ajaye, kwa ajili ya yule ajaye.”

101 Hilo ndilo jambo alilolifanyia Kanisa baada ya wao kupitia katika kuhesabiwa haki, kutakaswa. Yeye alilifanyia Kanisa lini? Yote hayo yalikuwa ni maagizo yaliyofanywa kwa imani na neema. Lakini kwenye—kwenye huduma ya Kipentekoste, Mungu aliwaita watu Wake waliotakaswa kifuani Mwake, kunyonya kutoka Kwake Uhai uliokuwa ndani ya Mungu uingie *ndani* yao. Huo hapo ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa ajili ya Kanisa, kama tu alivyomfanyia Ibrahimu. Hilo hapo Kundi teule la Kipentekoste wanaloliita walokole siku hizi, ninamaanisha Kundi teule.

102 Hao hapo, kama tu vile alivyoita kuhesabiwa haki, kutakaswa, na kumjaza Ibrahimu kwa nguvu Zake Mwenyewe, aliliita Kanisa kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa, na kulijaza Kanisa kwa nguvu Zake Mwenyewe, Roho Wake ndani ya Kanisa, na kulipa Kanisa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Huo ulikuwa ndio ninii kuu, hatua nyingine kuu iliyoipiga dunia, tunajua hilo. Martin Luther, John Wesley, na huduma ya Kipentekoste, hiyo imekuwa ndiyo huduma. Kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, sawasawa tu na alivyomfanyia Ibrahimu, Yeye ameufanyia Uzao wake baada yake. Mnalipata sasa?

103 Sasa, tieni alama kifungu cha 4 na cha 5 katika mlango uo huo hapo, katika wa 17. Sasa, ninawatakeni mwone kile Mungu alichofanya hapa. Yeye, Mungu hawezi kuzichafua sheria Zake Mwenyewe, hana budi kutimiza sheria Yake Mwenyewe. Kwa hiyo Mungu hawezi kuziasi sheria Zake Mwenyewe, hawezi kuzibatilisha sheria Zake Mwenyewe, na halafu, kusudi awe Mungu.

104 Sasa, kama tukiangalia, katika Agano la Kale kulikuwako, wakati mtoto alipozaliwa katika familia, mtoto huyo alikuwa, tuseme mvulana, alikuwa mrithi, bila shaka, lakini kabla mtoto huyo hajawa m—mrithi kabisa wa vitu vyote alivyokuwa navyo baba yake, kabla hajaingia mamlakani, kwanza aliwekwa chini ya mwalimu. Naye mwalimu huyu akamlea mwana huyu. Sasa, sisi—makasisi wote wanajua hilo, ya kwamba aliwekwa chini ya mwalimu.

105 Naye mwalimu huyu alikuwa ni mtu ambaye baba yake alimchunguza sana apate kumpata mtu aliye bora kuliko wote aliyeweza kumpata, kwa sababu huyo ni mwanawe, huyo ndiye atakayekuwa mrithi wake baadaye. Kwa hiyo basi anatafuta mwalimu mzuri, sio mwalimu atakayesema, "Vema, uh," kusema uongo na kusema, "loo, kanisa lako linaendelea vizuri tu. Maskini—maskini mtoto wa—wako anaendelea vizuri tu," wakati haendelei vizuri, yeye ni laghai. Hiyo, imezidi, ndiyo shida siku hizi ya maaskofu wetu wengi kupita kiasi, na kadhalika, na walimu wetu wote wa kujibunia, "Kanisa Lako linaendelea vema." Lakini ni uongo, haliendelei vizuri. "Wenye mfano wa utauwa, huku wakikana nguvu zake." Kuna kasoro mahali fulani.

106 Kwa hiyo wakati baba alipopata mwalimu bora kuliko wote angaliweza kumpata, mlezi bora kuliko wote, sasa, jinsi ambavyo hapana shaka huyo mwalimu aliona haya wakati alipoenda mbele ya baba yake, na kusema, "Loo, mwanao!"

107 "Yukoje? Mwanangu anaendeleaje?" Huyo baba alikuwa na shughuli nyingi, alikuwa na ufalme mkuu, na mengi, ingekuwa kama, mahali pengi, na wapangaji, na biashara ya kushughulikia.

108 Sasa, jinsi hapana shaka huyo mwalimu alivyojisikia alipokuja, akijua alikuwa ameajiriwa na huyo baba, akakaribia na kusema, "Loo, mwanao, hmm! Loo, yeye ni mbaya sana, si—siwezi kumfanya asikilize chochote, atakuwa na njia zake za kichwa ngumu, mtoto mwenye kichwa ngumu kuliko wote niliopata kuwaona maishani mwangu. Yeye ananinii tu, hatasikiliza. Nitaninii. . .Nina kitabu chako cha sheria hapa, ninaziweka moja kwa moja kwake, bali yeye anajua atakalofanya, mzee wake huenda akaiendesha kwa njia moja, bali yeye ataiendesha kwa njia nyingine." Jinsi ambavyo hapana shaka huyo mwalimu aliona haya wakati ilipombidi kuja na

kumwambia baba yake hivyo! Jinsi ambavyo hapana shaka baba alijisikia kulihusu, pia!

109 Na jinsi ambavyo Baba hana budi kujisikia siku hizi! Natumaini hili haliumizi, la kutosha tu kuwafanya mjiweke sawa, kwa kuwa saa yangu imekaribia kuwadia. Angalieni, lakini hili halina budi kusemwa, jinsi ambavyo Roho Mtakatifu alifanywa Mwalimu juu ya Nyumba ya Mungu, si askofu fulani anayetawala, si madhehebu fulani yanayotawala kwa mabavu, si baadhi ya nadharia hizi za kujibunia, mtoto wa Mungu anapaswa kumsikiliza Roho Mtakatifu, Maandiko ya Neno, mwana halisi wa Mungu, mwana halisi wa Ibrahimu.

110 Sasa, hapa ndipo wakati wa utengano unapokuja. Angalieni, "Loo," mnasema, "sisi ni Wapentekoste." Ulilitatua hapo, lakini ndio kwanza uanze tu basi. Unaona? Sasa, jinsi hapana shaka alijisikia! Jinsi Roho Mtakatifu hana budi kujisikia siku hizi kwenda mbele za Mungu Baba! Nawatakeni mniambie, kwenye Siku ya Pentekoste, je, Mungu alimchagua kasisi wa Kirumi kuwa Baba, Mwalimu? Je, alimweka wakfu askofu wa Kimethodisti? Mzee wa Kipentekoste? La, bwana, Yeye alimshusha Roho Mtakatifu awe Mtawala wa Kanisa. Kweli kabisa. Ilikuwaje kwake?

111 Yesu, akimtwaa Yohana, Naye alisema pale hatakufa, ndipo baadhi yao walisema Yeye alisema hivyo, bali Yeye hakusema hivyo. Kasema, "Itakuwaje kwa mtu huyu baada ya ufufuo?"

112 Kasema, "Inawahusu nini kama akikaa, hata nitakapokuja?" Lakini badala ya kufanya hivyo, kwa kuwa walisema hivyo, Yeye alimwinua tu, na kumwonyesha yote mpaka hapo alipokuja mwishoni mwa wakati wa kanisa. Kwa hiyo akaleta . . .

113 Kumbukeni, Yesu alisema, katika wakati wa pili wa kanisa, Smirna, kulikuwa na ma—matendo ya Wanikolai, na kile kilichokuwa matendo katika kanisa la pili, kikawa fundisho katika wakati wa tatu wa kanisa. Sasa, nini? Neno hilo halitumiki mahali pengine popote katika Biblia. Nililichunguza, nione lilikuwa ni nini, *nikao* maana yake ni "kushinda," *laitane* maana yake ni "walei," "kushinda walei."

114 Kumfanya mtu mtakatifu, mtu ambaye ni mtakatifu kuliko ulivyo wewe, kupanda tu na kumchukua mtu fulani, naye atakuwa nusu-mungu, ama kitu kama hicho, kusimama, nanyi mnafanya mtakayo, naye atasamehe dhambi, na hamna lingine, "kushinda walei." Kumwondoa Roho Mtakatifu Kanisani huko nje na kumweka wote jukwaani. Hiyo haikuwa njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo.

115 Hakuna mtu jukwaani aliye na haki ya kusema yeye ndiye pekee aliye na Roho Mtakatifu, naye ndiye pekee aliye na usemi katika hilo, Roho Mtakatifu ni kwa Mwili wote mzima wa Kristo,

kote huko nje, ambapo lugha, tafsiri, karama, madhihirisho ya Roho Mtakatifu. Lakini tulimshinda, hakika.

116 Kitu kile kile tulichotoka kwake, Pentekoste ilirudi moja kwa moja ndani yake tena, upesi tu walivyoweza kwenda. Kitu kile kile mlichokuwa mkiita, "maskini Wabatisti na Wamethodisti baridi," si—sio Wabaptisti baridi, Wapentekoste baridi sasa. Mlifanya jambo lile lile ambalo mlito-. . . baba zenu walitoka kwake, mligeuka moja kwa moja na kufanya jambo lile lile, mkamfungia kwenye chupa, mkafanya kanisa moja *hapa*, na lingine *huku*, na kupigana, mtu *huyu* asipokuja kanisani mwako, huna ushirikiano nalo.

117 Loo, ewe maskini, mnafiki, uliyerudi nyuma, *unayejiita* Mkristo, aibu kwako! Saa yako imekaribia. Mungu atawaadhibu kwa ajili ya jambo hilo, hakika kama nilivyo mtumishi Wake aliyesimama hapa, kuwatenganisha walei na kusababisha tofauti kati ya ndugu. Mungu aturehemu.

118 Sina kitu dhidi ya Wapentekoste, mfumo huo; sina kitu dhidi ya Katoliki, ni huo mfumo wa Ukatoliki; sina kitu dhidi ya Methodisti, ni mfumo huo; sina kitu dhidi ya Mlutheri, ni huo mfumo. Kuhesabiwa haki kwa Luther kulikuwa ni kwa kweli, bali walipokuwekea utaratibu kwa kukuundia dhehehebu, walikosea. Naye Wesley. . . Luther hakukuundia madhehebu kamwe, wale waliomfuata walifanya hivyo; Wesley hakukuundia madhehebu kamwe, wale waliomfuata walifanya hivyo; wala si wale waanzilishi wa Kipentekoste waliotoka kwenye upotovu huo, ni ninyi kundi lililowafuata mliofanya hivyo. Yale mliyofanya hasa, hapo ndipo tulipo leo hii.

119 Kama kanisa la Kipentekoste lingesimama miaka mia mbili kuanzia sasa, ninii. . . ma—mafanikio liliyopata ulimwenguni katika miaka hii thelathini iliyopita, ama arobaini, lingekuwa katika hali mbaya zaidi kuliko fundisho la Katoliki leo hii. Wakatoliki walianzia kwenye Pentekoste, pia. Ni kitu gani kilichosababisha hilo? Kuvuruga. Sasa, lakini Uzao wa kweli unabaki sawa.

120 Angalieni, vipi kama yule mwalimu, aliyemtunza huyo mtoto huko nyuma chini ya Agano la Kale. . . Loo, kama mtoto huyo alikuwa tu kama baba! Jamani, kila kitu alichosema baba: "Naam, ndivyo ilivyo. Amina. Hiyo ni kweli. Tutafanya hivyo."

121 Jinsi ambavyo hapana shaka mwalimu huyo alienda mbele ya baba yake, na kusema, "Mwanao ni mvulana mzuri sana. Mambo tu ufanyayo, hayo ndiyo afanyayo hasa, pia. Sijali vipi, una baadhi ya mabosi na wasimamizi huko nje, lakini, loo, jamani, hawamsumbui. Yeye anasimama imara, kama tu ufanyavyo wewe." Amina.

122 Jinsi ambavyo baba huyo hana budi kusema, "Huyo ni mwanangu! Ninamjivunia. Naam, bwana, yeye ni mwanangu. Siku moja nitauonyesha ulimwengu ya kwamba yeye ni

mwanangu." Vema. "Hawajali wakubwa dhaifu, yeye hudumu moja kwa moja na yale baba aliyosema."

123 Na jinsi ambavyo Roho Mtakatifu, leo hii, hana budi kujisikia anapoenda mbele za—za Baba na kusema, "Mbona, unajua nini? Wanawake Wa—Wa—Wako wanajipodoa, wanakata nywele zao. Wanaume Wako, uh, nanii Wako. . . Watoto Wako wanayaundia dhehebu makanisa ya msimamo mkali sana kama tu hao wengine, nao hawatashirikiana wao kwa wao," na mambo haya yote! Jinsi hana budi kujisikia! Jinsi ninii. . . Jinsi hapana shaka Mungu alijisikia kuhusu kanisa Lake! Jinsi hapana shaka ni fedheha!

"Mbona," Yeye akasema, "nilifikiri niliwaambia wakae nje ya Sodoma."

124 "Lakini walirudi moja kwa moja ndani yake, Baba." Kama tu Lutu, kwa ajili ya hela chache na mahali pazuri pa kuabudia, na jengo kubwa zaidi, na viti vizuri zaidi, na mhubiri aliyevalia vizuri zaidi, na mmoja kama huyu anayeweza kusema, "*Amina*," vizuri sana, kisha akaenda na kupata Ph.D., LL.D. nyuma ya jina lake, nao wanaweza kuwaambia wengine wote kuhusu *hili*.

125 Mungu hajali hata kidogo juu ya hilo, anataka mtu aliyejazwa na nguvu pamoja na Roho Mtakatifu, ambaye atasimama na kusema kweli, haijalishi kama inawachuna ngozi. Hiyo ni kweli. Lakini tunalipata wapi? Kila mtu ana tikiti ya posho na Kadilaki. Kuna kasoro mahali fulani. Kuna kasoro mahali fulani. Hiyo ndiyo sababu kanisa linayumbayumba siku hizi jinsi linavyofanya, kwa sababu limeondoka kwenye msingi.

126 Ilikuwaje wakati mwana huyo, basi, alipokuwa katika Agano la Kale? Ningependa kukaa hapo kwa muda kidogo, tutalirudia baadaye. Lakini sasa, vipi kama huyo mwana, basi, alikuwa mvulana mzuri, alikaa sawasawa kabisa na vile baba alivyokusudia iwe? Kama Biblia ilisema jambo moja, alidumu moja kwa moja nalo. Chochote Biblia ilichosema, yeye hudumu moja kwa moja nacho. Haidhuru ni kitu gani, haidhuru hao wengine wanaamini nini, wanyapara wote, yeye anadumu na Bosi mkuu, yeye hudumu na yale Mungu aliyosema. Mungu alisema, "Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe Kweli." Sijali kijacho wala kiendacho, dumu moja kwa moja nalo.

127 Nasi tunajua Biblia imetabiri ya kwamba wakati wa Kipentekoste utakuwa vuguvugu, utatapikwa kutoka katika kinywa cha Mungu, tunajua ya kwamba hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa, hatuna budi kukabiliana nalo, liko hapa.

128 Sasa, vema, sasa kama mwana huyu ni mwana mzuri, basi siku moja tuna, kile tunachoita katika Maandiko, Agano la Kale, kuwekwa kwa mwana, ama kunaitwa, wakati mwingine, sheria ya kufanywa mwana mwenye mamlaka. Sasa, mwana yuyu huyu aliyezaliwa katika familia, naye kamwe. . . alikuja. . . jina la—

lake halifai kwenye hundi, tungeliita hivyo, jina lake halifai huko nje bado, bado hajawahi kufanyiwa sheria ya kufanywa mwana mwenye mamlaka.

129 Lakini inapofikia wakati wa sheria ya kufanywa mwana mwenye mamlaka, baba anampeleka mwanawe mahali hadharani, na kumweka mahali fulani, na kumvika vazi fulani, na kufanya kile kinachojulikana kama kuwekwa kwa mwana, ama sheria ya kufanywa mwana mwenye mamlaka. Na sasa, mwana huyu anapofanywa mwana mwenye mamlaka katika familia yake mwenyewe, tangu wakati huo na kuendelea, mwana huyu anapewa mamlaka, ana kipaji, basi jina lake ni sawa sawa tu kama la baba lilivyo kwenye hundi, kwa sababu yeye ndiye bosi, yeye yuko juu ya hao wanyapara. Mungu humpa vitu ambavyo hakuna hata mmoja wa hao wanyapara aliyejua chochote kuvihusu, kwa sababu yeye ni mwana. Hiyo ni kweli.

130 Na hivyo ndivyo hasa Mungu alivyomfanyia Mwanawe Mwenyewe, baada ya kumthibitisha katika kila kitu. Basi kwenye mlango wa 17 wa Mathayo Mtakatifu, Yeye alimpandisha mlimani na kumfunika pale kwa—kwa Wingu la utukufu, na mavazi Yake yakang'aa kama jua katika joto lake, au, katika nguvu zake. Naye alipofanya hivyo, alisikia Sauti ikitoka Mbinguni, Petro, Yakobo, na Yohana, kasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa Naye, msikieni Yeye."

131 Alifanya nini? Aliiweka sheria, sheria Yake Mwenyewe ya kufanywa mwana mwenye mamlaka juu ya Mwanawe, akamweka Mwanawe mbele Yake. Haidhuru, "Yupo Musa, nilizungumza na Musa, kuna torati, kuna manabii, lakini huyu ni Mwanangu," sheria ya kufanywa mwana mwenye mamlaka. Loo, washika sabato na washika sheria, mna shida gani? "Huyu hapa Mwanangu, msikieni Yeye." Kweli.

132 Vema, hivyo ndivyo hasa Mungu alivyomfanyia Ibrahimu, Mwanawe hapo kabla, baada ya Ibrahimu kuhesabiwa haki kwa imani. Tunaamini hilo, sivyo? Uzao wa Ibrahimu, aliyehesabiwa haki kwa imani. Vema.

133 Jambo lililofuata lilikuwa basi, Yeye alifanya nini? Jambo lililofuata lilikuwa ni kutakaswa kwa Damu, kutakaswa kwa Damu kwa Mbegu; jambo lililofuata lilikuwa ni kunyonya nguvu za Mungu Mwenyewe ndani yake, kuingiza nguvu za Mungu Mwenyewe Kanisani. Yale aliyomfanyia Ibrahimu, aliufanyia Uzao wake baada yake. Kila mtu anaelewa hilo?

134 Vema, sasa angalieni, ndipo akamwambia Ibrahimu, angalieni jambo hili, kifungu cha 4 na cha 5, "Ibrahimu agano Langu sasa liko pamoja nawe." Amina. Ni hali ya jinsi gani hiyo ilipaswa kuwa! Ni Neno la kutia moyo jinsi gani kwa mzee wa miaka mia moja, moja kwa moja kwenye miaka mia moja, tisini na tisa, na kumwambia kwamba Yeye alikuwa ni El-Shadai, "Sasa ninakupa nguvu. Sasa nitakuweka pamoja Nami

sasa. Mimi ni Baba wa viumbe vyote, Jina Langu ni Elohimu." Mtu yeyote anajua ya kwamba neno *Elohimu* linamaanisha "yule—yule Ambaye Anajitosheleza kwa Yote, yu—yule mkuu Anayeishi kwa uweza wake Mwenyewe," Elohimu.

135 "Sasa, jina Langu ni Elohimu, na jina lako ni Abramu, wala hutaitwa tena Abramu, bali utaitwa Ibrahimu." Sasa ni wakati tutakapofikia mafundisho magumu sana sasa. *Ibrahimu*, angalieni, kutoka kwa *Elohimu* hadi kwa *Ibrahimu*, Yeye alimpa sehemu ya Jina Lake Mwenyewe, wakati alipomweka.

136 Angalieni, Ibrahimu na Uzao wake. Sasa, Mungu alipoliinua kanisa la Kipentekoste, alianza kuwaweka, akiwapa karama, na kadhalika, na kuwaweka katika Ufalme, lakini kila mtu alitaka kuwa na karama ile ile, na loo, jamani, hapo tukaenda. Kwa hiyo hilo haliuzuii Uzao wa Mungu, ninii tu, ama, Uzao wa Ibrahimu, unaendelea vivyo hivyo tu.

137 Angalieni, *Elohimu*, *Ibrahimu*, kampa sehemu ya Jina Lake Mwenyewe. Kwa sababu gani? "Nimekufanya baba wa mataifa," baba. "Nimekufanya baba wa mataifa mengi. Nami nitaweka sehemu ya Jina Langu pamoja na jina lako." Loo, jinsi ningeweza kufinyilia kitu fulani papa hapa sasa. Kampa sehemu ya Jina hilo: *Ibrahimu*. Kisha akabadilisha jina la Sara, maana alikuwa ni sehemu ya Ibrahimu.

138 Sasa angalieni, jambo lingine tunaloona limefanywa, hapa, ni katika mlango wa 18, mlango unaofuata, ambapo Mungu anamtokea Ibrahimu alipokuwa ameketi chini ya mwaloni. Sasa, Yeye, angalieni wakati Yeye, angalieni mahali alipomweka Mwanawe, kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kumpa karama. Sasa, alipomtokea kabla tu hajaiteketeza Sodoma . . .

139 Mimi si mpenzi wa kuangalia televisheni, kwa sababu ninapinga vipindi hivyo visivyokaguliwa. Lakini jana usiku, mahali nilipokuwa ninakaa, nilichukua kitabu baada ya kuingia nimechelewa sana, kisha nikaangalia kidogo, nikisoma kitabu pale, na kusema, *Mwongozo wa Televisheni*. Ndipo ikatokea niliona pale, kulikuwa na mahali ambapo walikuwa wakitaka kuonyesha haya makombora ya atomiki, ama *chochote kile*, kutoka Pentagon.

140 Kwa hiyo nikaenda kwenye redio hii, ama, televisheni, na kuifungulia kuangalia ko—kombora hili, nione jambo hili la atomiki, ninii, ama—ama, wanaviita visahani, vyovyote vile. Kumekuwa na ukosoaji mwingi, ubaya na uzuri mwingi, lakini sasa kuangalia kwa dakika moja tu. Kila mtu, una haki ya maoni yako, ninayo kwa yangu, hebu niyaelezee yangu.

141 Sasa, kabla Sodoma hiyo haijateketezwa, kabla tu . . . Wangapi waliona kipindi hicho? Nadhani wengi wenu mlikiona, vema. Si kitu kilichobuniwa tu, kilitoka serikalini. Nao wamekuwa kwenye hili, wakifanya utafiti huu kwa miaka mingi,

nao wanajua ya kwamba ni kweli kabisa. Ni kweli. Hilo si jambo jipya, kama wangesoma tu Maandiko, wangejua hasa mahali walipokuwa, haiwapasi kuwa na wasiwasi juu ya hilo. Lakini sasa, hebu na tuliweke hilo moja kwa moja kwenye ujumbe huu sasa, kwa dakika moja tu.

142 Sasa, wakati Ibrahimu, akiisha kuhesabiwa haki, kutakaswa, akampokea Roho Mtakatifu, Uzao wake namna hiyo, naye alikuwa amemweka mwana, mwana huyu alithibitisha kwamba alikuwa hivyo, maana alikuwa na Roho wa Mungu ndani yake, alifanya kazi zile zile, kile neno lake lilichokuwa, alikuwa sawa kabisa na Neno la Mungu.

143 Hatuwezi kamwe kujenga kanisa juu ya madhehebu mia tisa na kitu mbalimbali, huku kila moja likitofautiana na lingine. La, bwana. La, hatuwezi.

144 Sasa angalieni, lakini wakati mwana huyu, mwana wa Ibrahimu, Mzao, anapodhihirishwa, basi Roho wa Mungu katika Mzao huyo aliyedhihirishwa atafanya kazi zile zile ambazo Yesu alifanya, kwa sababu kazi zile zile za Uzao wa Kifalme zitakuwa katika Uzao wa Ibrahimu. Angalieni, kumweka mwana, kumfanya kama tu Mwana, Kanisa Lake.

145 Sasa, tunaposonga mbele, Ibrahimu akiwa ameketi chini ya mwaloni siku moja, aliangalia juu, naye akaona watu watatu wakimjia. Sasa liweke hili chini sasa, katika kumbukumbu yako: Yeye aliwaona watu watatu, walikuwa wamejaa mavumbi, labda, nao walikuja kutoka mbali. Ibrahimu akawaangalia, naye akatambua kuna kitu cha kiungu kuhusu hao watu, ukosi wao haukuwa umepinduliwa, labda, na kuvikwa vilemba virefu, ama wala hawakuitwa maaskofu, ama . . . lakini aliwaangalia, walikuwa ni watu wa kawaida tu, wamevalia tu kama watu wengine walivyokuwa wamevalia.

146 Ndipo Ibrahimu akamkimbilia, na kusema, "Bwana wangu, waweza kuingia na kuketi chini ya mti? Nami nitaleta maji kidogo, ukanawe miguu Yako, na—na nikupe kipande cha mkate, na ndipo uende zako." Ibrahimu alijua, sasa yeye alikuwa ni Uzao wa Ibrahimu. Sasa, kumbukeni, sikilizeni, Ibrahimu ndiye tu aliyetambua hilo.

147 Mlijua . . . ? Nilikuwa, nilizungumza na Myahudi hivi majuzi aliyeamini, sikuzote aliamini kuna Mungu mmoja, naye alitaka kuamini kunao watatu, kwa hiyo akasema, "Unajua hiyo ilimaanisha Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu hapo?" Loo, rehema, mtu anaweza kumwacha Mungu umbali gani? Ibrahimu kamwe hakusema, "Bwana zangu," alisema, "Bwana wangu," herufi kubwa B-w-a-n-a. Lakini Lutu, yule aliyerudi nyuma kule chini, alisema, "Bwana zangu," alipowaona wawili wao wakikwea, m-a-b-w-a-n-a.

148 Lakini yule mtu aliyetengwa, alijua wakati alipomwona, akasema, “Bwana wangu, Elohimu, njoo, ukaketi hapa chini.” Naye akamwendea.

149 Ndipo akaingia mbio na kumwambia Sara, “Kanda mkate upesi sana, wa unga, tunataka mikate.” Ki—kisha akatoka nje na kumchukua ndama aliyenona, nao wakamchinja huyo ndama, na kuandaa mambo, akakileta. Naye akaketi pale na kula. Wawili wao walishuka kwenda Sodoma kumhubiria Lutu huko chini Sodoma, na kulitoa kanisa hilo vuguvugu.

150 Sasa angalieni hayo matabaka matatu, sasa, kulikuwako na Lutu, na Sodoma, na Ibrahimu, walikuwa ndio matabaka matatu ya watu duniani siku hiyo. Sasa, tafadhalini sikilizeni kwa makini, hivyo ndivyo ilivyo leo hii kwa Uzao wa Ibrahimu. Mnaona? Kulikuwako na Sodoma, Wasodoma, ulimwengu, wenye dhambi; kulikuwako na kanisa vuguvugu lililounda dhehebu, limeketi pale chini, Lutu, dhambi za watu zikiitesa nafsi yake yenye haki. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema hasa. Haya basi, watu wengi wenye haki, wazuri huko chini, ambao wataitwa watoke, lakini sizungumzii hilo sasa hivi.

151 Sasa, walimtuma mtu huko chini kuwakomboa hao watu, naye akashuka na kuwahubiria, angalieni, kwa kanisa lililokuwa Sodoma, ulimwenguni. Sasa, wakati fulani juma hili, tutachukua *Alama Ya Mnyama Na Muhuri Wa Mungu*, na kuangalia jinsi hiyo ilivyoanza moja kwa moja huko Edeni, na kuja moja kwa moja ambapo Kaini alitoka Mbele za Mungu kumchukua mkewe, jinsi Sethi alivyokaa Mbele za Mungu na kumchukua mkewe. Jinsi ambavyo makanisa, kwa njia mbalimbali, yalitoka na madhehebu yao, yakitoka pamoja na madhehebu yao ya mfumo na kujipatia ka—kanisa, bibi-arusi, na huku Kanisa halisi, la kweli likikaa pamoja na Mungu, Bibi-arusi, kikamilifu.

152 Sasa, haya ndiyo yaliyotukia, wakati watu hawa waliposhuka kwenda kule...Na si ni ajabu jinsi alivyolibadilisha jina la Ibrahimu kutoka Abramu likawa Ibrahimu, ndipo yule mjumbe akashuka akaenda kule kuwahubiria watu hawa apate kuwatoa, na katika siku hii ya mwisho yule mjumbe aliyetumwa kwa hao Wasodoma, na kuwaita hao watu kutoka sehemu hizo huko chini anaitwa G-r-a-h-a-m? Sio B-i-l maradufu-y S-u-n-d-a-y, Sunday, lakini G-r-a-h-a-m. Mjumbe! Nionyeshe mjumbe mmoja wa kikanisa anayesimama mahali pake siku hizi, hakuna, mahali popote duniani kwa kanisa la Kikristo anayefanana na Billy *Graham*. Anafanya nini? Anapiga makelele, “Ondokeni kwenye kitu hicho. Mkajitenge,” kwa neno la kuhesabiwa haki, kuwaita watoke na kuwatenganisha.

153 Yeye alifanya nini? Ujumbe wake uliyapofusha macho yao wasiuone Mlango. Hivyo ndivyo ulivyofanya siku hizi. Ujumbe

huyapofusha macho yao, wana madhehebu mengi sana ndani yao, hawawezi kuuona Mlango, na Kristo ndiye huo Mlango. Kweli.

154 "Loo," wanasema, "vema, mimi ni Mmethodisti." "Vema, angalia hapa, Bw. Graham, mimi ni Mpresbiteri." "Mimi ni Mlutheri." "Mimi..." Hawauoni Mlango. Nao Ujumbe umeyapofusha macho yao. Hivi hamwoni mwujiza wa Mungu? Mnaliona kundi la Lutu? Huko mbali Sodoma.

155 Sasa, angalieni, kwa huyu Mmoja aliyebaki nyuma kwa Kanisa teule, Mmoja. Yeye alisema...Sasa angalieni, siku chache tu kabla ninii la Ibrahimu...Jina la Abramu lilikuwa limebadilishwa likawa Ibrahimu. Sasa, kamwe Yeye hakusema, "Abramu, yu wapi S-a-r-a-i mkeo?" Alisema, "*Ibrahimu*, yu wapi S-a-r-a mkeo?" Alijuaje hilo kama Yeye alikuwa ni Mgeni?

156 Sasa, angalieni, Yeye anazungumza na Uzao mteule sasa, wa Ibrahimu. Sasa, Yeye anazungumza na Ibrahimu, na kama alivyofanya kwa Ibrahimu, Yeye hana budi kumfanyia ule Uzao baada yake; tumepata, kila kitu, kikamilifu mpaka wakati huu. "Ibrahimu," ufunuo, "yuko wapi Sara, mkeo?"

Kasema, "Yuko hemani nyuma Yako." Sasa, kumbukeni, "nyuma Yako."

157 Akasema, "Nitakuzuru," *Mimi*, hicho kiwakilishi nafsi kilihusishwa, mnaona, "Nitakuzuru," hivyo ndivyo alivyojua ni nani, jina lake lilikuwa...Yeye Ndiye aliyelibadilisha jina lake, "Ibrahimu, nitakuzuru, katika muhula wake Sara. Nami nitamtuma mtoto huyu, kama tu vile nilivyosema nitafanya." Unaona? "Nitafanya hivyo."

158 Basi Sara aliposikia hayo, sasa, dada zangu humu ndani, ninyi wanawake vijana samahani jambo hili, lakini Sara alicheka. Mnajua ni kwa nini alicheka? Alisema, "Mimi, mwanamke mkongwe, niwe na raha tena na bwana wangu, yeye akiwa mkongwe pia?"

159 Sasa, kama mume na mke, kwa—kwa kuwa uhusiano wa familia ulikuwa umekoma kwa miaka mingi, walikuwa na umri wa miaka mia moja. Akasema, "Mimi, ati niwe tena msichana, niishi na mume wa—wangu pale, nasi tuwe na raha pamoja, kama vijana, watu waliofunga ndoa?" Ndipo likamchekesha, naye akasema, "Ati mimi, mwanamke mkongwe, niishi na mume wangu huko nje, tena, wakati hatujakuwa na maisha ya namna hiyo, labda kwa muda wa miaka kumi na mitano, ishirini." Mnaona? "Sisi...Hiyo ingewezekanaje?"

Naye alipocheka, basi yule Malaika, huku amegeuza mgongo Wake, akasema, "Kwa nini Sara akacheka?"

160 Yesu alirejea kwake, na kusema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake

Mwana wa Adamu." Ndivyo itakavyokuwa kwa Uzao wa Ibrahimu.

161 Mnaweza kuona mahali Lutu anapoketi? Mnaweza kuona mahali Ujumbe ulipo? Mnaweza kuona Ujumbe ambao umeenda kwa Kanisa teule? Nguvu za Mungu zimerudi miongoni mwa watu, Mungu akiishi katika mwili wa kibinadamu wa Kanisa Lake Mwenyewe, akifanya ishara zile zile, nao wanaiita kusoma akili, telepathia ya kiakili, kupiga ramli. Si ajabu wamehukumiwa. Si ajabu makombora yameelekezwa kule, wanavyoyaita, hewani, wala hawajui lolote kuyahusu.

162 Nitawapa maelezo yangu juu yake: Malaika ndio wameshuka, kama walivyofanya kule Sodoma. Mnajua, ninaamini tulikuwa na picha ya mmoja upande wa nyuma, kwenye picha moja hapa mahali fulani, itakuwepo, mkutanoni siku chache zijazo. Linaye roho yeye yule, hufanya mambo yale yale. Roho yuyo huyo Kanisani atafanya mambo yale yale aliyofanya Yesu.

163 Nasi tunaangalia. Na kwenye Pentagon, wanapofika kule, nao wangeweza kuona hayo makombora yakiwazunguka, namna hiyo, sio kitu cha kujibunia, hadithi fulani ya uongo, ni kweli kabisa, hawa hapa kwenye rada, hawa hapa wamepigwa picha na—na kamera. Nao wana mbio sana hata wangetoweka tu. Einstein alithibitisha, kabla hajafa, kama makombora mawili yalikuwa yakija kasi vya kutosha, ama watu wawili wakishuka barabarani kwa motokaa, wangeweza kuwa wakija upesi vya kutosha, wangeweza kupitiana moja kwa moja, bila hata kusumbuana, wakija upesi sana, lakini ingechukua mabilioni ya maili kwa sekunde kufanya hivyo, lakini wangefanya hivyo.

164 Mwangalieni Yesu, ha—hatuwezi kulielewa, wakati Yesu alipoingia chumbani kupitia u—ukuta wa mawe, milango ikiwa imefungwa, na kusimama pale, baada ya kuwa na mwili Wake uliotukuzwa, na kula nyama. Haleluya! Utukufu! Nena kuhusu wakati wa angani, Kanisa linajiandaa kuchukua mmoja. Upesi! Huku wakijivuna ati ndege zao zinakwenda kasi sana, "Tuna mtu ndani ya sputniki." Mbona, jamani! Hiyo inaleta tofauti gani kwa Kanisa la Mungu aliye hai? Masalaale!

165 Yeye alisema, "Mambo haya yatakapotukia, inua kichwa chako, kutakuwako na ishara katika mbingu juu, na katika nchi chini, bahari ikivuma, matetemeko ya nchi mahali mahali, huo ndio wakati, anzeni kuangalia juu, ukombozi wenu unakaribia."

166 Mnaona ishara za Sodoma, madhehebu ambayo yamelipeleka kanisa huko nje katika siri, loo, njia ya kujihesabia haki, ya kisheria, lakini huyo mwanamume na mwanamke anayengojea ahadi ya Mungu anayo ishara ikitenda kazi miongoni mwao, huku Mungu wa kweli, aliye hai, akiyatambua mawazo yenyewe ya moyo, ni Neno. Yesu alikuwa Neno.

167 “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwako pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu,” Yohana Mtakatifu 1. Hiyo ni kweli? Waebrania mlango wa 4 ilisema, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, likitambua hata mawazo, na makusudi ya moyo.”

168 Na wakati Neno, wakati Neno la Mungu, sio nusu Yake, sehemu Yake, iliyochanganywa na kanuni fulani ya imani ya kujibunia, “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo, nalo litatendwa,” bali wakati Neno la kweli linapodhihirishwa ndani yako, Hilo ni Mpambanuzi wa mawazo ya moyo. Nao watu wanaiita kusoma akili, telepathia ya kiakili.

169 Si ajabu walimwita Yesu *Beelzebuli*. Naye akasema, “Ninawasamehe. Lakini Roho Mtakatifu atakapokuja na kufanya hivyo, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe.” Ndipo mnaona ni kwa nini jina letu liko kwenye kombora linaloning’inia kule, mahali fulani. Mnaona mahali hukumu inaposimama. Angalieni, hakika tumeangamia.

170 Hilo hapo kundi la Billy Graham kule chini, likimhubiria Lutu huyo, “Ondokeni Sodoma. Ondokeni Sodoma. Ondokeni Sodoma.” Labda huyo mvulana hajui, nijuavyo mimi, ama, mtu huyo, nafikiri ana umri wa kama miaka thelathini na saba, ama arobaini, la, kama arobaini na nne, ama chochote kile, arobaini na mitano, sijui Billy ana umri gani. Kasema . . . Vema, anafikia mahali fulani kwenye umri wa miaka arobaini. Lakini hata hivyo, jinsi mtu huyo, labda, hatambui ni nini. Mnaona? Huyo hapo, yeye ndiye mjumbe wa siku hizi kwa kanisa hilo, bila kutambua ilibidi aitwe namna hiyo. Jinsi yeye . . . kila kitu . . .

Unasema, “Jina hilo lilikuwa na uhusiano gani nalo?”

171 Kwa nini Yeye akabadilisha jina la Yakobo? Kwa nini akabadilisha majina hayo mengine yote walipomjia? “Jina lako linaitwa Simoni, tangu sasa utaitwa Petro.” “Wewe ulikuwa Sauli, bali utaitwa Paulo tangu sasa na kuendelea.” Vipi kuhusu majina haya yote, kama hayamaanishi kitu fulani?

172 “Loo,” mnasema, “hiyo ni elimu ya tarakimu, ibilisi anayo moja.” Hiyo ni kweli, na Mungu ana moja. Kila kitu alicho nacho ibilisi, amekiiga kutoka kwa Mungu. Kweli kabisa.

173 Akabadilisha jina lake. Baada ya Yesu kushinda, Yeye alipokea Jina jipya, Mwenyewe, kila mshindi. Kanisa, litakaposhinda kabisa, ufunuo wake unaanza kuwa halisi Kwao. Kwa nini Yeye akaitwa hivyo? Kwa nini Yeye ni Mjumbe siku hizi? Kwamba wakati mtu anapokuwa ndani, kama tu ilivyokuwa katika Edeni, alijiangamiza mwenyewe kwa maarifa yake mwenyewe, na leo hii, anafanya jambo lile lile, akijiangamiza kwa maarifa yake mwenyewe.

174 Angalieni sasa, dakika chache tu kabla hatujafunga, tunaninii, kweli tuna dakika thelathini, bali sio lazima

tuzichukue. Angalieni, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Sasa, alishuka akaenda na kuhubiri, hao Malaika walihubiri, Huyu mwingine alibaki nyuma, Mjumbe.

175 Mhudumu fulani aliniuliza wakati mmoja, "Ndugu Branham, ati ulisema huyo alikuwa ni Mungu?" Huyo alikuwa ni Mungu, Ibrahimu alimwita Elohimu. Ukitaka kubishana na Ibrahimu, Biblia, hiyo ni sawa. Lakini alisema ilikuwa ni Elohimu, alisimama pale na akala nyama, amevaa nguo za kawaida, akala nyama, akanywa maziwa ya ng'ombe, akala mkate, akatoweka mbele ya Ibrahimu. Alikuwa Elohimu. Akithibitisha nini? Wakati Yesu aliporejea jambo hilo, kwamba Elohimu angerudi katika Uzao wa Ibrahimu katika siku za mwisho, "Na kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma," kwa Kanisa teule, "ndivyo itakavyokuwa."

176 Na kwa kanisa lililoko Sodoma, ndivyo itakavyokuwa. Sasa, tunaona mahali wanaposimama, sivyo? Tunaona majina, kila kitu, yamewekwa sawa kabisa, kikamilifu kabisa mahali tunapoketi. Alifanya nini basi? Mara baada ya hayo, kama nilivyochukua hili mara nyingi, ninaamini niliwahubiria juu yake wakati mmoja, aliubadilisha mwili wa Ibrahimu na Sara, na kuwarudisha kuwa kijana mwanamume na mwanamke. Sasa, tu—tunajua ya kwamba hiyo ni kweli.

177 Sasa, kumbukeni. . . Sasa, hebu niwathibitishie papa hapa, ili kwamba ninyi, uh, kama mkipata mawazo yoyote kwamba walikuwa, "Katika siku hizo waliishi tu muda mrefu zaidi." Biblia ilisema hapa ya kwamba wote wawili walikuwa na umri mkubwa, wenye umri mkubwa. Basi kwa nini Sara akasema kwamba "Kama ningeweza kuwa na raha na bwana wangu"? Naye Ibrahimu, Biblia ilisema ya kwamba mwili wake ulikuwa kama uliokufa, mbegu mwilini mwake ilikuwa kama iliyokufa, halafu miaka arobaini na mitano baada ya Isaka kuzaliwa, alikuwa na watoto wengine saba. Hebu jibu hilo, utaweza?

178 Kwa nini Abimeleki akampenda—Abimeleki akampenda, Sara, basi, wakati alipokuwa mwanamke mkongwe? Kasema, "Mimi, mwanamke mkongwe, mwenye umri mkubwa, mimi, mkongwe, kama nilivyo sasa, ningeweza kupata raha tena?" Ndipo alipofunga safari ya maili mia tatu, akashuka kule, na kumwona mfalme kijana, alimpenda, kitu kizuri sana alichopata kuona. Yeye aliubadilisha mwili wake. Kwa nini? Ilimbidi kuubadilisha mwili wake kusudi ampokee mwana aliyeahidiwa. Na hilo ndilo jambo linalofuata katika utaratibu, kule kubadilishwa kwa mwili, kule Kunyakuliwa.

179 Sasa, vipi kama angalimchukua tu Ibrahimu, kasema, "Sasa, Ibrahimu, nitakurudisha tu kuwa kijana mwanamume, nitamrudisha Sara awe kijana mwanamke, na sasa, ninyi nyote endeleeni tu mkamzae huyo mwana"? Wasingefanya hivyo, maana waliishi pamoja walipokuwa vijana, wala hawakumpata

huyo mwana, hawakuwa na mwana yeyote, nao walikuwa wameishi pamoja miaka hii yote, kama angaliwabadilisha tu warudi. Ilibidi kuwe na aina tofauti ya badiliko. Loo, utukufu! Ati nini? Asingeweza kuingia katika utungu wa kuzaa akiwa na moyo wenye umri wa miaka mia moja, mishipa ya maziwa ilikuwa imekauka mwilini mwake, tumbo lake la uzazi lilikuwa tasa. Loo, najua linaonekana la kigeni, najua linaonekana hivyo. Linaonekana la kigeni.

180 Ungeweza . . . ? Vipi kama mtoto mchanga, kabla hajazaliwa, wakati akiwa ndani ya tumbo la uzazi la mama yake, angeweza kusema, “Loo, ole wangu! Wananiambia nitazaliwa katika siku chache. Nitafanya nini? Wananiambia kuna ulimwengu mkubwa, kuna mwangaza wa jua, watu wanatembea huku na huku. Loo! Nitafanyaje . . . ? Ni nini ambacho . . . ? Nitapataje riziki? Ninapata riziki yangu kutoka mumu humu tumboni. Nafasi hiyo yote kubwa, nitafanya nini? Ole wangu”? Lakini laiti angeliweza kuwazia ilikuwa ni nini, laiti angeninii . . . Ukiisha kutoka nje upande huu mara moja, halafu uangalie nyuma, kamwe hutaki kwenda kwenye hilo tumbo la uzazi tena.

181 Na hivyo ni kama tulivyo sasa, tukiliwazia, “Hiyo itakuwaje? U—ulimwengu mwingine ni upi, ambapo tunaweza kupita kutoka Utukufuni?” Mbona, wakati wanapoweza kuchukua darubini na kuona miaka milioni mia moja na ishirini ya anga ya nuru, hiyo si moja ya kumi na sita ya inchi katika Umilele. Haleluya! Utukufu! Lakini Yesu alikuja duniani kutoka Mbinguni katika wazo. Utukufu! Nalo Kanisa litakuwa vivyo hivyo, litapita nuru kwa kasi sana! Utukufu kwa Mungu.

182 Unasema, “Inawezekanaje?” Ni kama tu, ninajuaje sasa? Jambo pekee nijualo sasa ni inchi, na yadi, na maili, na siku, na majuma, na saa, na dakika, hivyo ndivyo tunavyokadiria, tuko katika tumbo la uzazi la dunia. Lakini ngojeni mpaka tutakapozaliwa mara moja Ng’ambo ya pili. Utukufu! Ngojeni mpaka badiliko hili litakapokuja. Naam. Halafu nafasi ya kuja kama ninii . . . kutoka ninii, Utukufuni, hapa mara moja, nusu muda, kasi hivyo, tupitie moja kwa moja ukutani, hata hatujui upo. Haya basi. Mambo haya ya duniani yatakuwa rahisi sana wakati huo. Ni—ni . . . Loo, jamani, hakutakuwa na kitu kwake. La, bwana.

183 Wakati mwili wa Ibrahimu ulipobadilishwa, mwili wa Sara ulipobadilishwa, kama vile kamwe haukuwa umebadilishwa hapo awali. Sasa, sote tunajua ya kwamba Yesu atakapokuja, tutatwaliwa katika Unyakuo, nasi tunajua miili yetu itabidi ibadilishwe kwanza. Na itaninii . . . Na haitabidi kuwa, kurudi tu kwa vijana wanaume na wanawake, lakini itabidi ibadilishwe, kwa sababu ilibidi mwili wa Ibrahimu na Sara ubadilishwe kwa njia ambayo wangeweza kumpokea mwana aliyeahidiwa.

184 Huyo ni Ibrahimu, ilibidi mwili wake ubadilishwe apate

kumpokea mwana aliyeahidiwa, akisha kuhesabiwa haki, kutakaswa, kujazwa na Roho Mtakatifu, akaitwa kwa uteuzi, akamdhihirisha Mungu wa Utukufu katikati yake, ndipo basi mwili wake ukabadilishwa kusudi ampokee mwana aliyeahidiwa.

185 Vema, Kanisa limepitia katika kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, karama zikadhihirishwa Kwake. Na sasa nini? Roho wa Mungu akitenda kazi Kanisani, akifanya kazi zile zile alizofanya Yesu kabla hajaondoka, kama ahadi. Na kitu kinachofuata ni nini? Kule kubadilishwa. Jambo lingine lililompata Ibrahimu, lilikuwa ni mwili uliobadilishwa, ilimbidi awe nao, la sivyo kamwe asingempata huyo mwana. Basi jambo linalofuata kwa Kanisa ni Kunyakuliwa.

186 Itabidi tubadilishwe na kunyakuliwa ili kumlaki hewani. Hatuwezi kumlaki duniani, hatuna budi kwenda hewani kumlaki. Ni Mwana ajaye, Mwana aliyeahidiwa. Amina. Tumemtazamia sasa, kwa mamia ya miaka, Yeye atakuja siku moja. Lakini jambo linalofuata kwa Kanisa ni kubadilishwa. Tumekuwa na kila ishara: kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuwekwa kwa Mwana, kudhihirishwa kwa Roho. Sasa, nini? Kubadilishwa kwa mwili kwa ajili ya Kunyakuliwa.

187 Loo, jamani! Jinsi Kanisa linavyopaswa kuwa likipunga mikono yake katika utukufu, likimshukuru Mungu, likimshukuru Mungu! Dakika yoyote kule kubadilishwa kunaweza kuja, kwa kuwa Biblia ilisema kutakuwa kwa ulimwengu mzima, Yesu alisema, "Watu wawili watakuwa kwenye kinu, wakisaga, nitamchukua mmoja, na kumwacha mmoja; wawili kondeni, nitamchukua mmoja, na kumwacha mmoja; wawili kitandani," ilionyesha itakuwa pande zote mbili za dunia, wakati ni usiku upande mmoja, iwe mchana upande huo mwingine, "Nitamchukua mmoja, na kumwacha mmoja." Kunyakuliwa kutakuwa kwa watu wote, na miili yao itabadilishwa.

188 Itabidi miili yetu ibadilishwe, kamwe hatuwezi kubadilika kuwa vijana wanaume na wanawake, hatuna budi kuwa na mwili wa aina nyingine, ili tuweze kunyakuliwa hewani kumpokea Mwana aliyeahidiwa. Hilo ndilo Kanisa linangojea sasa, Kanisa la kweli. Kila dhihirisho, yale aliyomfanyia Ibrahimu, ameufanyia Uzao wake baada yake, akiacha jambo moja, hilo ni Kunyakuliwa kwa Kanisa.

189 "Na mtakapoona mambo haya yakianza kutimia," Yesu alisema, "inua kichwa chako. Angalia juu! Ukombozi wako unakaribia." Wakati Yesu aliporejea hilo, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika Sodoma," mtakapomwona Billy Graham mambo leo akishuka kwenda Sodoma, mtakapoona ishara zikianza kuonekana mbele ya Kanisa teule, na hayo mengine

yakilipiga vita, angalieni, wakati wa Kunyakuliwa umewadia. Mtini ukichipusha majani yake huko ng'ambo, kizazi hicho hakitapita mpaka yote yatimie. Nalo limeingia sana kwenye kizazi hicho, tangu Wayahudi wamekuwa wakirudi kwenye nchi ya uenyeji wao. Tuko katika wakati wa mwisho.

> Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
> Ishara ambazo manabii walitabiri;
> Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
> na hofu;
> "Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu."

190 Njoo, uende pamoja nasi huko Miami, wakati mtu aliyesimama na mkono wake huko Greenland, apate kuachilia mabomu ya atomiki ambayo yangeangamiza nusu ya dunia, akatetemeka, kisha akawa Mkristo, atakuwa akitoa hotuba. Wakati alipoona kombora kwenye skrini, nao wakadhani ilikuwa ni Urusi ikianza. Tuko tayari, pia, mataifa mengine yako tayari, pia. Castro akitumiwa huko chini, kama tu ki—kibaraka, akicheza ili Urusi iweze kuingia mle karibu vya kutosha, wanaweza kurusha makombora yao ya atomiki na kadhalika, haya hapa moja kwa moja chini ya pua yetu.

191 Nazo karama za Mungu, dhihirisho la Mungu miongoni mwa watu Wake, zikifanya jambo lile lile alilofanya Yesu Kristo zimeenea ulimwenguni kote sasa. Mnaona? Liko tayari. Sasa, jambo linalofuata ni kule kubadilishwa, na kutwaliwa hewani kumlaki.

192 Kule kubadilishwa, kwa wale wanaomtazamia Mwana aliyeahidiwa. Je, mnamtazamia alasiri ya leo, mkingojea? "Loo, nitakuwa nikiangalia na kungojea, kuona tamasha hilo; Yeye yuaja tena." "Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu."

193 Mbona dunia hii italipuliwa vipande vipande moja ya hizi. . .Loo! Ingeweza kutukia kabla ya asubuhi. Kuna Jambo moja tu, hilo ni Mwenyezi Mungu, angeweza kutuzuia tusije tukalipuliwa vipande-vipande, lakini katika saa nyingine moja tangu sasa, Urusi imetupita kwa mbali sana katika sayansi. Na kama yule mfafanuzi wa habari alivyosema hivi majuzi usiku, si Urusi inayofanya hivyo, wala si wanasayansi wetu, Wajerumani ndio wamefanya jambo hilo. Katika vile vita, tulichukua baadhi yao, nao wakawachukua wengine, na haya basi.

194 Wana mtu sasa anayeenda, anayesimama katika kifaa kidogo, kitu kama sputniki, hapa juu duniani. Vipi kama, huenda wakawa na mamia ya hao, vipi kama wangejongea tu juu ya Marekani, na kusema, "Jisalimisheni, la sivyo muwe majivu." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .jisalimisha, bila shaka. Ingekuwaje? Hawa hapa Warusi wangekuja, kutoka kwenye nyumba zenu, mnajua ambacho kingetukia.

195 Wasipojisalimisha, inakuwaje? Majivu yanakuja. Hilo lingeweza kutukia lini? Katika saa nyingine moja kuanzia sasa. Lakini kumbukeni, kabla hilo halijatukia, hapa ndipo hamkubali, bali kabla hilo halijatukia, Yesu yuaja kwa ajili ya Kanisa. Kabla chembe moja ya Moto kushuka juu ya Sodoma, ilibidi Lutu atoke; kabla tone moja la mvua kunyesha, ilibidi Ibrahimu awe ndani ya, ninamaanisha, ilibidi Nuhu awe ndani ya safina. Na kama ilivyokuwa katika siku za Ibrahimu, ama, siku za Nuhu, na katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu. Kabla jambo lolote halijatukia, Kanisa linaenda katika Kunyakuliwa Kwake. Amina. Wako ndani ya Kristo, tayari wamehukumiwa.

196 Na moja ya asubuhi hizi, kutakuwako na kutoweka, na moja ya siku hizi usiku, kutakuwako na kutoweka, nalo Kanisa litabadilishwa, na kunyakuliwa kumlaki Yesu hewani. Na ole kwa kundi hili basi! Watasaga ndimi zao kwa sababu ya maumivu, wakati atomiki zitakapoingia nchini, ziyachome macho yote, na kutiririka kama maji, na ndimi zinasagwa kwa maumivu, na kupiga mayowe, bomu likilipuka tu moja baada ya lingine. Mtakumbuka ilikuwa ni kiasi gani cha telepathia ya kiakili, ilikuwa kundi la watakatifu wanaojifingirisha kiasi gani, ama la walokole. Kumbukeni, Mungu anajua anachofanya. Naam, bwana.

197 Jambo lingine linalongojewa ni yule Mzao wa Ibrahimu aliyeteuliwa, na aliyeitwa atoke, Yule ambaye ametambua dhihirisho la Mungu miongoni mwa watu Wake na kusimama, akingojea, huyo Ndiye atakayenyakuliwa kumlaki Yeye hewani.

198 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu. Kama kuna wale hapa leo hii wasiomjua Yeye kama Mwokozi binafsi, kwamba hujajazwa na Roho Mtakatifu, kwamba ufunuo wa Mungu haujawahi kuyagusa maisha yako, nawe ndio kwanza ujiunge na kanisa, na uliishi maisha mazuri, yaliyonyooka, unajua ya kwamba wale Waebrania huko nyuma, hao makuhani, waliishi maisha makamilifu, hakuna mtu angaliweza kuyawekea kidole maisha yao, walikuwa watu watakatifu, waliotakaswa, naye Yesu akasema, "Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi"?

199 Dhambi ni nini? Ni kutokuamini. Kutokuamini nini? Neno la Mungu. Sasa, hilo ni Neno la Mungu kwa Ibrahimu na Uzao wake baada yake. Kama hujajulikana kwa Mungu kama Mwanawe, kwa kuzaliwa mara ya pili upate kujazwa na Roho Wake, hujapata kunyonya kutoka kwa El-Shadai, kifua cha Mungu, kwa nini usije papa hapa na kusimama hapa? Hebu tuombe pamoja nawe, wakati ndugu wahudumu wakiwa huku kuomba.

200 Utasimama sasa? Ninaamini saa ya kushawishi huku kwote imekwisha tu. Hujampokea Kristo na kujazwa na Roho, njoo. Maskini mtu mmoja anaenda madhabahuni, na huyo

ni Myahudi, aliye karibu na Mwethiopia. Mungu aturehemu. Mnawezaje kulisikia Neno la Mungu na halafu mkae kimya? Enyi marafiki, hivi hamwoni ya kwamba sayansi ilisema, yapata miaka mitano iliyopita, ni usiku wa manane kasoro dakika tatu?

201 Mnajua kile Mungu alichofanya? Alinyosha mkono, wakati umepita, aliunyosha mkono Wake na kuvisimamisha. Yeye anashikilia wakati mkononi Mwake Kanisa lipate kujiweka tayari. Kuna washiriki wengine wachache ambao hawajaingia bado, wa Mwili wa Kristo, labda mmoja wao yuko hapa leo, hiyo ndiyo sababu niko hapa, hiyo ndiyo sababu nimeongozwa hapa, ni kujaribu kuwashawishi. Sisemi, "Sasa usiwe Mkatoliki, usiwe Mmethodisti." Sisemi *kule* unakopaswa kuwa, wewe kuwa mfuasi wa hayo yote ama usiwe wa yoyote yao. Lakini ninawatakeni mjazwe na Roho Wake, kama hujajazwa, wewe ni . . .

202 Kumbukeni tu, nitakutana nanyi siku hiyo, na maneno haya yatakuwa shahidi dhidi yenu. Yote yako kwenye kanda ya Mungu iliyorekodiwa, na kwa kamera Yake kuu ya picha. Nanyi mkiketi, huku nanyi mkiondoka na kuliacha, utajiona mwenyewe siku hiyo katika kioo cha Mungu. Utakuja?

> . . . kuwa na njia Yako Mwenyewe!
> Wewe ndiwe Mfinyanzi;
> Mimi ndimi . . .

Sahau tu kila kitu sasa, njoo, "Mimi ni udongo."

> Nifinyange na unifanye
> Upendavyo,
> Wakati nikingojea,

Je, umejitolea?

> Nimejitolea . . .

203 "Mapenzi Yako na yatendeke, Bwana. Ondoa ukanisa wote kutoka kwangu. Ondoa ugumu wote na madhehebu yote kutoka kwangu, Bwana. Hebu niwe Mkristo halisi."

> . . . Bwana!
> Uwe na njia Yako Mwenyewe!
> Shikilia utu wangu
> Mamlaka yote!
> Nijaze na Roho Wako
> Hata wote watakapomwona
> Kristo pekee, daima,
> Akiishi ndani yangu!

> Fanya . . .

Mungu akubariki, mama. Njoo moja kwa moja mbele, Dada.

> Kuwa na njia Yako Mwenyewe!
> Wewe ndiwe Mfinyanzi;

Ninyi nyote Wakatoliki, Wabaptisti, Wapresbiteri, Wamethodisti, Wapentekoste!

> Nifinyange na unifanye
> Upendavyo,
> Ninapojitolea,
> Nimejitolea na kutulia.

> . . . njia Yako Mwenyewe, Bwana!

204 Sasa, wakati watu wanaposhuka, wangali wanakuja, mradi tu watu wanakuja, tutaushikilia. Sidhani tuna wakati mwingi zaidi, katika ulimwengu huu, kufanya miito ya namna hii.

205 Sasa, kumbukeni tu, ninanena katika Jina la Bwana: Saa inakuja ambapo mtapiga makelele mpate mkutano kama huu. Hutakuwa na shauku sana ya kuamka na kutoka nje, utakuwa umechelewa sana wakati huo. Utatoka nje vema, uingie Umilele bila Mungu, bila . . .

206 Mnaniita ninii wenu . . . nabii, kamwe sijiiti hivyo, ninyi mnaniita. Nalo Neno la Bwana lilikuja wapi? Neno *nabii* linamaanisha nini? "Mfunuzi wa Kiungu wa Neno la Kiungu, lililoandikwa." Halafu una fasiri yako mwenyewe, na kuichukua juu ya Neno halisi. Ishara na maajabu yanathibitisha kama ni kweli ama si kweli. Mungu aliwaambia jinsi ya kuyatambua, "Kama wanayosema yakitimia, basi ni kweli, kama sivyo, si kweli." Sasa, wewe jiamulie mwenyewe.

207 Afadhali umkimbilie Mungu, Mpentekoste, wakati ukiwa na nafasi ya kufanya hivyo. Usichukue tu wazo fulani kwamba "Nilinena kwa lugha, na hilo linamaanisha yote." Hiyo ni mbali tu kama Wamethodisti kupaza sauti, Walutheri wakipeana mikono. Afadhali umjie Mungu.

> Wakati nikingojea,
> Nimejitolea . . .

208 Sasa kumbukeni, baada ya ujumbe huu, alasiri ya leo, niko huru na damu ya watu wote, mkutano umetolewa Chicago, nimewaambia BWANA ASEMA HIVI, nimewathibitishia kwa Maandiko ya kwamba tuko mwisho. Sasa, sina hatia ya damu ya mtu yeyote tangu sasa.

209 Sijui ni Wakristo wangapi, huko nje, wangekuja madhabahuni, na kuomba pamoja na watu hawa hapa, waliosimama kwenye madhabahu, na kuomba? Yeyote wenu Wakristo, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, angetaka kuja hapa juu, na kuomba pamoja na watu hawa?

> . . . mimi na kunifanya
> Upendavyo,
> Wakati nikingojea,
> Nimejitolea na nimetulia.

210 Ibrahimu na Uzao wake baada yake, Ibrahimu na Uzao wake. Hebu niwaambieni jambo fulani. Siku chache

tu zilizopita nilikuwa California katika kanisa kubwa la kimadhehebu, dhehebu la Kipentekoste, watu wachache walikuja madhabahuni, wanne ama watano, baada ya kuhubiri ujumbe mgumu, halafu wenye dhambi wanne ama watano wakakimbilia madhabahuni, wakianguka mmoja juu ya mwingine. Ilinibidi kuwasihi na kuwashawishi watu waje waombe pamoja nao. Nilifanya hivyo kwa kusudi fulani alasiri ya leo, nione ni nani angekuja huku, na miongoni mwa watu kama mia tatu, angalieni wale waliokuja kuomba.

211 Mbona, Wabaptisti wa Kentucky kule chini milimani, nilikozaliwa, wangewafanya Wapentekoste wajionee aibu, hebu mtu mmoja asimame aje kuelekea madhabahuni, kutakuwako na kanisa zima limemzunguka moja kwa moja, wakijaribu kuninii. . .namshukuru sana Mungu kwamba nafsi moja imeingia. Na halafu ati sisi ni Uzao wa Ibrahimu, tumepoteza bidii yote tuliyopata kuwa nayo. Mnaona ninalomaanisha? Ee Mungu!

212 Na tuinamishe vichwa vyetu. Kwenu ninyi watu hapa madhabahuni, ninawatakeni myasalimishe maisha Kwake sasa. Kumbukeni, nitakutana nanyi asubuhi hiyo, nitatoa hesabu ya ujumbe huu alasiri ya leo. Nimekuwa Chicago tangu mwanzo wa huduma yangu, kwa kuwa inakwisha sasa. Siwezi kuwa nabii na mwinjilisti kwa wakati mmoja, huduma moja itachukua mahali pake hivi karibuni.

213 Na wakati baada ya wakati, jinsi ambavyo nimekuwa hapa Chicago, na kusimama saa baada ya saa, moyo kwa moyo pamoja nanyi, mumewahi kunisikia nikiwaambia lolote katika Jina la Bwana, ila lililokuwa ukweli? Kama ndivyo, ninawaomba mje mlisahihishe. La, bwana, haijulikani. Basi ninawaambia, katika Jina la Bwana, chini ya hali kama hiyo: Kama ukija hapa juu leo, Mungu alikuongoza hapa, hii ndiyo saa ya ukombozi wako, kama utaamini kwa moyo wako wote. Ninawatakeni tu, kwa unyenyekevu tu, kukiri tu kila kitu ambacho mmefanya ambacho ni makosa, mbele za Mungu, useme, "Mungu, samahani kwa jambo hilo. Na sasa nipo hapa, nikikutaka Wewe unipe ubatizo wa Roho Mtakatifu. Lijalie."

214 Na tunapofunga ibada, pamoja nanyi madhabahuni hapa, mkiomba, nitaliomba hili kusanyiko, na wote, kusimama katika maombi. Mkiwekeana mikono, madhabahuni hapa, ninyi watu mlio na hawa.

215 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea Wewe, alasiri ya leo, ma—matunda, ama, masazo, nchi imevunwa muda mrefu uliopita, nasi tunaokota masazo kama Ruthu. Jinsi ndugu zetu wainjilisti wanavyojua mambo haya vizuri! Ndugu yetu Tommy Hicks hapa, Ndugu Oral Roberts, na Billy Graham, na jinsi ambavyo—ambavyo wanajua ya kwamba tunaokota masazo tu

Marekani, tuone kama tunaweza kupata ubua *hapa*, ama *pale*. Tunajua mwisho umekaribia.

216 Baba Mungu, hawa waliokuja, Wewe umesema katika Neno Lako, "Yeye anijiaye Mimi, sitamtupa nje kamwe." Na pia, "Kwamba hakuna mtu awezaye kuja, asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote wanijiao Mimi, nitawapa Uzima wa Milele, na kumfufua katika siku ya mwisho." Hiyo ni ahadi Yako, Bwana. Na kama mtumishi Wako, na matunda ya ujumbe huu, ninakupa Wewe hawa wanaotafuta madhabahuni, ninawakabidhi Kwako, Bwana, kama mtumishi Wako, katika maombi.

217 Na pamoja na hawa watumishi Wako wengine wote, wanaosimama hapa, ambao ni mashahidi wa kufufuka Kwako, mashahidi wa nguvu za Mungu, nasi tumesimama hapa, kwa kilindi, Bwana, kwa uaminifu kutoka moyoni mwetu, tukiamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu, tukiamini ya kwamba Wewe unakuja, na mambo haya yote ya kutisha tunayoona na kusikia, mataifa yanatetemeka, na kuona Israeli wakienda kwenye nchi ya uenyeji wao, mataifa yanafadhaika, tukiona vitu vya kisiri juu ya Washington, mambo ya kutisha juu ya nchi, fadhaa ya wakati, na dhiki kati ya mataifa.

218 Dhiki, dhiki kubwa sana, wote wana wasiwasi sana hata hawajui la kufanya, kila mmoja akiwa na silaha za atomiki na haidrojeni, zimefichwa kisiri, akimngojea tu huyo mwingine kuchukua hatua. Siku moja kosa, vodka kali kupita kiasi itanywewa ama chochote kile, ndipo kombora litarushwa liingie kwenye skrini, basi hili hapa linaenda. Mungu, Wewe uliahidi jambo hilo, nami ninakuamini.

219 Nuhu alisimama mlangoni mwa safina, na kuwahubiria watu waliokuwa wakifa. Na leo hii, mtu halisi wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili anasimama Mlangoni pa Yesu Kristo, na kuwaonyesha watu Njia ya kutokea, si kanisa, si dhehebu, bali Mlangoni, Kristo. Jalia watu hawa waje Mlangoni sasa hivi, wakibisha Mlangoni. Tunajua kutakuwako na mkono unaokaribisha utakaonyoshwa, na kusema, "Njoni, enyi mliobarikiwa na Baba Yangu, ingieni katika furaha mliyoandaliwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, maana hakuna mtu angaliweza kuja, ila wale aliowajua tangu zamani." Nao wamekuja alasiri ya leo, nami ninawakabidhi Kwako, kama mtumishi Wako, na kama watu Wako. Tujalie, Bwana, kwa kila mmoja wao, katika Jina la Yesu Kristo.

220 Na wakati kila mtu humu ndani, ninyi watu mlio karibu na madhabahu, kwa imani, kwa imani, sio lazima uhisi jambo moja, lakini moyoni mwako. . . Sasa, ulikujaje hapa? Mungu, huko nyuma kwenye kusanyiko, alikuvuta huku juu. Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Naye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele." Na kuna aina moja tu ya

Uzima wa Milele, hiyo ni Roho Mtakatifu. Sasa, kama utaamini, kwa moyo wako wote, kwamba Mungu atakupa Roho Mtakatifu, inua mikono yako, na kusema, "Asante, Bwana, nimekuja hapa sasa kumpokea."

Ninyi nyote huko nje kwenye kusanyiko mnaoamini pamoja nao, inueni mikono yenu, na kusema, "Bwana, tuko tayari kwa ajili ya Roho Mtakatifu."

221 Ndugu Tommy Hicks, ninakutaka uje, na kuomba sasa, juu yao, papa hapa. Naam, bwana. Wote. . .?. . .

61-0423 Ibrahimu Na Uzao Wake Baada Yake
Stephen Mather High School
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org